epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatatu Julai 8, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581731
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

UKURASA WA 5
**Saba** mbaroni tuhuma kutapeli benki zaidi mil. 300/-

UKURASA WA 7
**Zaidi** ya 400,000 wafikiwa msaada kisheria Kampeni ya Samia



UKURASA WA 19
**CCM** yampongeza Aweso hatua kusimamisha kazi vigogo DAWASA



UKURASA 22
**KROOS AMUOMBA RADHI RAFU PEDRI**



# KASI NDOA KUVUNJIKA

• **Mchawi** mkuu huyu hapa; ndoa moja...*Endelea ukurasa 2*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akimuonesha Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Sekondari Wilaya wa Halmashauri ya Mufindi, Daniel Mapilya dawati ambalo limetengenezwa chini ya viwango wakati alipokagua ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Iramba katika Halmashauri ya Mufindi mkoani Iringa jana. Wa tatu kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Peter Serukamba.
**PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

## Hofu yatanda madai watoto kutekwa

UKURASA 3

## Washikiliwa tuhuma za kuiba nyaya njia ya treni SGR

UKURASA 19

TADB
*"Benki ya Wakulima"*



*Mkurugenzi wa Benki ya Maendeleo ya kilimo ya Tanzania Frank Nyabundege*

## TADB YASHIKA NAFASI YA PILI MIONGONI MWA TAASISI ZA FEDHA ZA MAENDELEO ZA SADC

HABARI UKURASA 5

# KASI NDOA KUVUNJIKA

## -Mchawi mkuu huyu hapa; ndoa moja...

**Na Christina Mwakangale**

RIPOTI ya Utafiti wa Ufuatiliaji wa Kaya (NPS) 2020/21 iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inaonesha asilimia 57 ya Watanzania hawako katika ndoa.

Hata asilimia 43 ya walio katika ndoa nao wanakabiliwa na balaa. Shida kuu ni kwamba 'taasisi ndoa' imetikiswa.

Wataalamu wa saikolojia na wahadhiri wameeleza kiini cha wanandoa kutodumu, wakinyooshea kidole malezi duni kwa watoto kwa kizazi cha sasa na ukuaji wa teknolojia kuwa ndiyo mzizi wa tatizo.

Wamesema zipo athari katika maisha yao baadaye ukubwani hasa katika ndoa au uhusiano, kwamba wanapokumbana na changamoto wanazikabili na si kurudi kwa mama au baba kupata maelekezo.

Msaikolojia Tiba wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Dk. Isaac Lema, anasema kuwa hivi sasa ni kawaida kwa mtu mzima (mwenye umri wa kuanzia miaka 18) mwenye familia, akiwa na changamoto za kifamilia hasa wanandoa kurudi kwa mzazi kuchukua maelekezo badala ya ushauri.

"Unakuta mtu ana kisa na yuko katika ndoa, anampigia simu mama yake, tunataka tununue gari wewe unasemaje? Unakuta kijana huyu kujitegemea katika uamuzi wake ni tatizo.

"Kila umri una rasilimali unazohitaji, ukimpa mtoto rasilimali maarifa kulingana na umri wake maana yake umemsaidia," alisema Dk. Lema.

Alisema kuna pengo kati ya malezi na jamii, huku familia ikiachiwa jukumu hilo pekee,



wakati familia hizo hivi sasa nazo zinaandamwa na changamoto za kutafuta maisha zaidi.

"Kazi ni kile kinachozalishwa kuliko muda unaotumika kwenye kazi yenyewe. Kila hatua ya malezi inamsaidia mtoto kujitegemea, ili afikapo miaka zaidi ya 18 aweze kujitegemea.

"Malezi yanahitaji muda, kujitoa, mpangilio, kupanga ni kuchagua. Uangalie kazi ya mwajiri, lakini pia malezi, maisha ya kila siku. Kama una majukumu ya kikazi pia utenge muda wa malezi, ni sehemu ya kazi zako za kila siku.

"Unapokuwa nyumbani unapika, kwanini usimshirikishe mtoto aje karibu umwelekeze namna ya kupika? Unapokwenda kwenye mazoezi kwanini usiende naye ajifunze?" Dk. Lema anasema.

Mtaalamu huyo anasema mtoto anapohusishwa katika shughuli tofauti pamoja na mzazi au mlezi, inaongeza utamaduni wa kuwasilisha jambo na changamoto anazokumbana nazo.

"Mtoto akiweza kujitegemea ndivyo unavyopata muda na wewe wa kufanya kazi zingine. Malezi ni kazi, kazi ya mwajiri unaweza kupeleka nyumbani lakini kazi ya malezi huwezi kupeleka kazini.

"Mtoto lazima awe na mipaka. Mtoto ili asisumbue unampa simu kama namna ya kumdhibiti, ili asikusumbue badala ya kumhusisha kile unachokifanya, anajifunza taratibu," alifafanua.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu Dodoma (UDOM), Dk. Jabhera Matogoro, anasema kipindi cha likizo kwa watoto ni muda mzuri kwa wazazi na walezi kuzungumza nao ikiwamo kuwapa muda wa wao kutoa maoni.

"Ni kweli tuko 'bize' ila lazima kuweka uwiano katika maisha. Tunapotenga muda wa kuzungumza na vijana inasaidia kujua ukuaji wao.

"Katika dunia iliyojaa majukumu na teknolojia, lazima hatua hii ichukuliwe ili kukupa muda kufahamu familia na ukuaji wa akili na kuchukua hatua kwa wakati sahihi.

"Nilihudhuria mjadala UDOM, mwasilishaji mada akazungumza kwamba malezi yanaweza kuchangia ama kuathiri ukuaji wa mtoto.

"Matumizi ya teknolojia yanaongeza familia kujitenga, huku baba akiwa na chombo chake cha mawasiliano, yaani simu, mama na mtoto hivyo hivyo, jambo hili linasababisha kuwapo wigo miongoni mwao.

"Utakuta mtu ameingia katika uhusiano mpya ama ndoa, ikafika wakati kukawa na tofauti na uhusiano huo ukakoma, utakuta mmoja alikuwa na picha, uhusiano unapokoma anaanza kuziachia picha ambazo mlipiga awali, hii ina athari, teknolojia inaathiri," anasema Dk. Matogoro.

Anasema majukumu ya kikazi yasiwe kikwazo kwa familia kujitenga katika malezi, akisema teknolojia itumike kumhusisha mwanafamilia kama baba au mama, aliye mbali na upeo wa macho yao, kwa kuungana kupitia teknolojia ya mawasiliano ili kukuza ukaribu.

Agness Andrew (56), mkazi wa Mwananyamala, mkoani Dar es Salaam, anasema wazazi kutoa maelekezo kwa watoto wao baada ya kuona au kuolewa hutokana na sababu nyingi.

"Malezi ya siku hizi mengi yanaegemea kwetu kinamama... umelea watoto wako pengine baba wala hakutoa mchango wowote. Watoto wanaona, mama nimehangaika kuwasomesha, baadaye huwa na uchungu na kuniamini sana mama yao.

"Mimi nilimwambia kijana wangu akioa awe na mke mwenye heshima na kupenda wazazi wa pande zote mbili. Siyo mwanangu kaoa, mwanamke ndipo anampanda kichwani. Hata mimi huku ananisahau, nani atavumilia?" Agness anahoji.

Kwa mujibu wa ripoti tajwa ya NBS, wanandoa waliotengana nchini ni asilimia tano, waliopeana talaka ni asilimia 1.9, wasiowahi kuwa katika ndoa ni asilimia 38.9, wajane na wagane ni asilimia 5.4 na wanaoishi kiuchumba ni asilimia 6.1.

Utafiti huo wa NBS pia unaonesha kuwa idadi ya wasioishi katika ndoa vijijini ni asilimia 55.5 ya waliofikia umri wa kuoa au kuolewa, huku mijini ni asilimia 61.5 sawa na tofauti ya asilimia sita.

Kwa mujibu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), kwa mwaka 2019 talaka nchini zilikuwa 442, mwaka 2020 ulikuwa na talaka 511 na mwaka 2021 zilikuwa 550.

Takwimu za RITA zinaonesha kuwa mwaka 2019, ndoa 43,479 zilisajiliwa huku mwaka 2020, zikisajiliwa ndoa 54,071, mwaka 2021 ndoa 49,000 na mwaka 2022 ndoa 51,011.

Vilevile, takwimu za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum zinaonesha kulikuwa na migogoro ya ndoa 39,571 katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Aprili 2022. Kati yake, migogoro 19,262 ilipata suluhu, 15,718 ilikuwa katika usuluhishi na 4,576 ilikuwa mahakamani.

Utaratibu wa kisheria unaelekeza kukishakuwa na mgogoro katika ndoa, wanandoa wanapaswa kuanzia kwa Ofisa Ustawi wa Jamii ambako ikishindikana, ndiko hupewa baraka za kufikisha mgogoro huo mahakamani.

**GARI INAUZWA**

**T340 XXX Toyota Hilux Double Cab White Mwaka Iliyotengenezwa - 2013**

Ofa zinaalikwa kwa gari hapo juu. Gari linapatikana Ipuli – Tabora na laweza kukaguliwa Ipuli, Tabora siku za kazi kuanzia **saa 3:00** kamili asubuhi hadi **saa 10:00** Jioni, hadi Aprili.

Mwisho wa ukaguzi ni tarehe **20-07-2024.**

**Kwa ukaguzi piga simu: +255 747 900 261**
Wanunuzi wanaovutiwa wanaweza kutuma ofa zao ikiambatana na jina na namba ya simu kwa email **info.ceylextz@gmail.com**

**Subject iwe**
**OFFER HILUX DOUBLE CAB T340**

**INVITATION FOR TENDER**

The Goethe-institut Tanzania is inviting tenders for comprehensive security services at our premises located at 63 Alykhan Road, Upanga, Dar es Salaam. As the culture institute of the Federal Republic of Germany, we promote German language and culture worldwide. We require a security provider for 24/7 on-site presence, nightly patrols advanced remote surveillance, and additional event security personnel. The contract term is one year, starting in 2024, with an extension option. Proposals must include company credentials, security protocols, emergency response times, and a detailed fee structure. Interested parties should submit proposals by **{submission date 05/08/2024.}** For full tender details, visit www.goethe.de/daressalaam or contact Alpha Parsalaw at **alpha.parsalaw@goethe.de.**

## HABARI KITAIFA

# Hofu yatanda madai watoto kutekwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mtaa wa Soko la Wakulima, Kata Ruanda jijini Mbeya, wameingiwa hofu baada ya kundi la watu wasiojulikana kuanza kuwateka watoto wao, huku ikidaiwa kusafirishwa kwenda kuuzwa nje ya nchi.

Aidha, wananchi hao wanahusisha utoroshaji huo wa watoto na biashara haramu ya viungo vya binadamu na kuiomba serikali iwasaidie kukabiliana na tatizo hilo.

Waliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye mtaa huo baada ya mmoja wa watoto hao aliyekuwa amepotea kwa zaidi ya siku 10 kupatikana, huku ikidaiwa kuwa waliomteka walitaka kumuua ili wauze viungo vyake.

Mtoto huyo (jina limehifadhiwa) alisema akiwa maeneo ya jirani na nyumbani kwao walikuja vijana wawili ambao walimtuma akawanunulie vocha ya simu dukani.

Alisema aliporudi walichukua vocha kisha wakamkamata na kumfunga kitambaa usoni na kuondoka naye mpaka kwenye pagala moja ambalo hajui lilipo na huko alifunguliwa kitambaa, lakini akafungwa mikono na miguu.

Alisema kwenye pagala hilo alimkuta mtoto mwingine mmoja ambaye hamfahamu akiwa amefungwa mikono na miguu na muda wote huo walikuwa wanaishi kwenye pagala hilo kwa kupewa maji pekee.

Alisema alibaini kuwa watu hao walikuwa na nia ya kuwaua na kuuza viungo vyao kutokana na simu walizokuwa wanawasiliana na watu ambao hawawajui. "Niliwasikia wakizungumza kwenye simu wakisema 'kila kiungo kinakuwa na bei yake' baada ya hapo wakaondoka na hatukujua walikokuwa wanakwenda, mwenzangu alikuwa hawajamfunga vizuri ndipo akafanikiwa kufungua kamba akanifungua na mimi tukaanza kukimbia," alisema mtoto huyo na kuongeza:

"Nilipofika barabarani nilimuona dereva bodaboda nikamuomba anisaidie kumpigia simu mama kwa sababu nilishika namba yake na alipompigia akamuelekeza nyumbani na akamuomba anilete ndipo nikaletwa mpaka hapa nyumbani," aliongeza.

Alisema mwenzake ambaye walikuwa naye walikuwa hawafahamiani na baada ya kufungua walikimbia kila mmoja uelekeo wake kwa hiyo hajui mwezake alikwenda wapi.

Mmoja wa wananchi wa eneo hilo, Malema Mpila, alisema kabla ya mtoto huyo kupotea, watu wasiojulikana walimteka binti yake mwenye umri wa miaka 25 pamoja na rafiki yake na wakatokomea nayo kusikojulikana, lakini baadaye walifanikiwa kuwaokoa.

Alisema watoto hao walichukuliwa wakasafirishwa kwenda Mbozi, mkoani Songwe ambako walikuwa wamefungiwa kwenye moja ya nyumba na walipofanya ufuatiliaji kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi waliwaokoa.

Alisema waliambiwa watoto hao walikuwa kwenye harakati za kusafirishwa kwenda Uarabuni kwa ajili ya kutumikishwa kwenye kazi za ndani pamoja na biashara ya viungo kama figo, maini na moyo.

"Kwa hiyo jamani hii biashara ipo ndiyo maana mimi niliposikia kwamba mtoto huyu amepotea nilihangaika sana kuzunguka na picha yake na hawa watekaji wana tabia ya kuwahamisha hamisha watoto wanaokuwa wamewateka ili wasigundulike," alisema Malema.

Mkuu wa machifu wa Jiji la Mbeya, Chifu Rocket Mwashinga aliwataka vijana wa mtaa huo pamoja na wa maeneo yote ya jiji hilo kuacha kujiingiza kwenye biashara hiyo haramu ya uuzaji wa binadamu.

Alisema biashara hiyo inafanywa zaidi na wanaume na kuwataka wanawake kusaidia kuwafichua wahalifu hao ili wasiendelee na tabia hiyo.

Pia, aliwataka mabinti wanapoolewa wahakikishe wanajua kazi wanazofanya waume zao.

Polisi Kata wa Kata ya Ruanda, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Fatma Hamdan, aliwataka wazazi kuwalinda watoto wao dhidi ya vitendo hivyo na ukatili mwingine wowote ambao umekuwa ukitokea kwenye jamii.

Alisema atamhoji vizuri mtoto huyo ili wapate taarifa zaidi na wajuwe namna ya kushughulika na vitendo hivyo ambavyo alidai kuwa kwa mujibu wa sheria ni haramu.


**NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA-MWANZA-MAOMBI YA UTEKELEZAJI Na. 69/2020
SIDNEY THOMAS KAZI ..............................................MSHINDA TUZO
DHIDI YA
MARGARITHA THOMAS KAZI ..........................................MSHINDWA TUZO
M/MWANZO YA KISESA- SHAURI LA MADAI Na. 108/2022

INSP. NYAMWAILA ______________________________MDAI
DHIDI YA
YUSUPH MANASE ______________________________MDAIWA

M/MWANZO YA KISESA- SHAURI LA JINAI Na. 179/2022

INSP. NYAMWAILA ______________________________MDAI
DHIDI YA
YUSUPH MANASE ______________________________MDAIWA

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA-MWANZA, MAHAKAMA YA MWANZO KISESA, TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI AMBAZO NI NYUMBA MBILI (2). MNADA UTAFANYIKA MAHALI MALI ILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 01 | NYUMBA 01 PLOT NA.249 BLOCK "U" - JIJI LA MWANZA | MITI MIREFU, NYAMAGANA-MWANZA | 06/08/2024 SAA 2:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 02 | NYUMBA 01 ILIYOPO KITONGOJI CHA IGUDIJA 'A' KATA YA KISESA WILAYA YA MAGU | IGUDIJA 'A'-KISESA | 07/08/2024 SAA 2:00 ASUBUHI NA KUENDELA |

**MASHARTI YA MNADA;**

1. KWA MALI INAYOHAMISHIKA, MSHINDI WA MNADA ATALIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA MARA BAADA YA KUTANGAZWA MSHINDI.
2. KWA MALI ISIYOHAMISHIKA, MSHINDI ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
3. MTEJA ANATAKIWA KUKAGUA MALI KABLA YA MNADA KUANZA.
4. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0768-588155**



**Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com**

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha **Nipashe** au **The Guardian** kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

TANGAZO

tigo pesa

# Ni Zaidi ya Pesa

## Ada za wateja. Piga *150*01#

| Kiwango (Tsh) | | Kutuma pesa kwenda Tigo Pesa | Kutuma pesa kwenda Mitandao washirika | Kutoa pesa kwa Wakala/ATM | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzia | Mwisho | Ada ya Tigo Pesa | Ada ya Tigo Pesa | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato |
| 100 | 999 | 15 | 15 | - | 10 | 10 |
| 1,000 | 1,999 | 30 | 45 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000 | 2,999 | 30 | 45 | 400 | 10 | 410 |
| 3,000 | 3,999 | 50 | 90 | 600 | 14 | 614 |
| 4,000 | 4,999 | 60 | 90 | 650 | 27 | 677 |
| 5,000 | 6,999 | 130 | 180 | 950 | 54 | 1,004 |
| 7,000 | 9,999 | 150 | 180 | 1,000 | 56 | 1,056 |
| 10,000 | 14,999 | 360 | 495 | 1,450 | 102 | 1,552 |
| 15,000 | 19,999 | 360 | 495 | 1,450 | 195 | 1,645 |
| 20,000 | 29,999 | 380 | 540 | 1,850 | 306 | 2,156 |
| 30,000 | 39,999 | 400 | 612 | 1,850 | 351 | 2,201 |
| 40,000 | 49,999 | 410 | 675 | 2,350 | 419 | 2,769 |
| 50,000 | 99,999 | 720 | 1,125 | 2,700 | 573 | 3,273 |
| 100,000 | 199,999 | 1,000 | 1,440 | 3,650 | 707 | 4,357 |
| 200,000 | 299,999 | 1,200 | 1,710 | 5,300 | 821 | 6,121 |
| 300,000 | 399,999 | 1,500 | 2,070 | 6,500 | 838 | 7,338 |
| 400,000 | 499,999 | 1,500 | 2,250 | 7,000 | 982 | 7,982 |
| 500,000 | 599,999 | 2,200 | 2,880 | 7,500 | 1,245 | 8,745 |
| 600,000 | 699,999 | 3,300 | 3,870 | 8,000 | 1,532 | 9,532 |
| 700,000 | 799,999 | 3,300 | 3,870 | 8,000 | 1,700 | 9,700 |
| 800,000 | 899,999 | 3,500 | 3,870 | 8,000 | 1,750 | 9,750 |
| 900,000 | 1,000,000 | 3,500 | 5,400 | 8,000 | 1,776 | 9,776 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 5,000 | 5,400 | 8,000 | 1,875 | 9,875 |
| 3,000,001 | 10,000,000 | 5,000 | 5,400 | 10,000 | 2,000 | 12,000 |

| Tukio | Kuanzia | Mwisho | Ada |
|---|---|---|---|
| Kuweka pesa | 1,000 | 5,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwa mteja ambaye ana akaunti ya mitandao washirika | 100 | 5,000,000 | Ada ya kutuma |
| Kutoa pesa kwa mteja ambaye hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwenda nchi za nje | 100 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |
| Malipo kwa Tigo Pesa | 500 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |

| Tukio | Ada |
|---|---|
| Kubadilisha namba ya siri | BURE |
| Kuangalia salio/ Taarifa ndogo | 50 |
| Kurudisha muamala uliokosea (Jihudumie) | 50 |
| **Kupata taarifa ya mwezi** | **Ada** |
| Taarifa ya Mwezi jana/Mwezi huu | BURE |
| Taarifa ya Miezi 3 | 1,000 |
| Taarifa ya Mwaka 1 | 2,000 |

Kwa vigezo na masharti ya huduma tembelea tovuti: https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-standard-terms-and-conditions. **Ada zote zimejumuisha kodi zote zinazohusika**
Kwa Ada za huduma nyingine tembelea **tovuti; https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-tariffs**

**Furahia Malipo kwa Tigo Pesa:** Lipa kwa simu

**KUMBUKA:**


1. Unaweza kuweka au kupokea hadi TSh 5,000,000 kwa siku na unaweza kutoa au kutuma hadi TSh 5,000,000 kwa siku, pia unaweza kuhifadhi hadi TSh 10,000,000 kwa wakati mmoja kwenye akaunti yako ya Tigo Pesa, kama usajili wako umekamilika.
2. Onesha kitambulisho chako kabla ya kuweka au kutoa pesa kwa Wakala.
3. Hakikisha taarifa zako za usajili ni sahihi kwa kupiga *106# kisha 2 au piga huduma kwa wateja kwa maelezo zaidi.
4. Hesabu pesa zako na hakikisha salio lako la Tigo Pesa linaendana na muamala uliofanya kabla ya kuondoka kwa Wakala.
5. Kila mara unapotuma pesa, kumbuka kuhakiki namba ya mpokeaji kuepuka kukosea na usumbufu.
6. Hakikisha unahifadhi namba yako ya siri (PIN), simu yako na laini yako kwa usalama. Usimpe (PIN, Simu, laini yako) wala kumtajia mtu yoyote namba yako ya siri, iwe Wakala wa Tigo Pesa, mfanyakazi wa Tigo au mhudumu wa Tigo Huduma kwa wateja. Pia kumbuka kubadili namba yako ya siri mara kwa mara.
7. Tigo itakupigia kwa 100 Tu.
8. Kutoa taarifa yoyote dhidi ya udanganyifu Piga simu namba 100 au tuma ujumbe kwenda namba 15040 au barua pepe kwenda customercare@tigo.co.tz
9. Unaweza kupokea pesa kutoka nchi zaidi ya 200 duniani, na unaweza kutuma pesa kwenda nchi zote za Mashariki na Kusini mwa Afrika .
10. Kupata vigezo na masharti ya kutumia Tigo Pesa, tembelea duka la Tigo lililopo karibu nawe au www.tigo.co.tz

Unaweza kurudisha **muamala uliokosea, token ya luku, ku-unbar akaunti yako ya Tigo Pesa** na **kuriseti PIN**

Piga ***150*01#**
chagua **6 (Jihudumie)**
kisha chagua huduma unayotaka

tigo pesa

App yenye urahisi wa kushangaza!




**Fanya malipo ya Serikali**

TRA DAWASA TANESCO LUKU RITA

Pakua kwenye

Google Play App Store

tigo pesa

www.tigo.co.tz

Kuwasaliana na huduma kwa wateja,
Piga **100** bure au tembelea duka lolote la Tigo!
Ada hizi ni kuanzia 01 Julai 2023

tigo

# Saba mbaroni tuhuma kutapeli benki mil. 305/-

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATU saba wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wametiwa mbaroni na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za utapeli wa Sh. milioni 305 katika Benki ya CRDB.

Wanaotuhumiwa ni pamoja na meneja wa benki hiyo tawi la Kahama, Erick Chambanenge, wafanyakazi wawili wa benki hiyo na wengine wanne, ambao wanadaiwa kufanya utapeli huo jijini Dar es Salaam.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, ACP Kennedy Mgani, jana alithibitisha tukio hilo akisema lilitokea Julai 4, mwaka huu majira ya saa saba mchana.

Alisema siku hiyo lilifika gari dogo aina ya IST na kupaki nje ya benki ambako alishuka mwanamke ambaye hakumtaja jina kwa sababu za kiuchunguzi na kuingia moja kwa moja hadi kwa meneja wa huduma kwa wateja na kumweleza shida yake naye kumkabidhi kwa mfanyakazi mwingine ili amhudumie.

Mgani alisema baada ya kukabidhiwa alihudumiwa na kufanikiwa kutoa Sh. milioni 30 tasilimu kwa kutumia kadi bandia na baadaye alitoa tena Sh. milioni 275 kutoka kwenye akaunti nyingine, ambazo ziliingizwa kwenye akaunti mbili tofauti za wateja wa benki hiyo.

Kutokana na tukio hilo, alisema wanawashikilia watuhumia saba wakiwamo watumishi hao wa benki pamoja na wengine wanne wanaodaiwa kuwa matapeli kutoka jijini Dar es Salaam.

"Wote wanatuhumiwa kwa utapeli wakiwa na kadi bandia, hakuna fedha yoyote iliyopotea kwa sababu Sh. milioni 30 waliyokuwa nayo tumeikamata na kuzuia muamala wa Sh. milioni 275 waliokuwa wakiufanya kwa wakati huo," alisema Mgani.

Aidha, alisema jeshi hilo lilipokea taarifa ya siri kuhusu mpango huo wa utapeli na kuweka mtego ambao ulifanikisha kukamata wakiwa na Sh. milioni 30 na watumishi watatu wa benki hiyo ambao pia wanadaiwa kushirikiana kufanikisha utapeli huo.

ACP Mgani aliwataka watumishi wa taasisi za kifedha kuacha tabia ya kushirikiana na wahalifu ambayo inawaondolea imani wateja wao pamoja na taasisi husika.

Aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kutoa taarifa za uhalifu maeneo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kufuatilia akaunti zao katika taasisi za kifedha kujua uendeshaji ili kama kutakuwa na utofauti watoe taarifa haraka.

Kamanda Mgani alisema uchunguzi unaendelea kubaini mtandao mzima uliohusika na utapeli huo kwa kushirikiana na maofisa wa benki hiyo na watakaobainika watafikishwa mahakani kujibu tuhuma zinazowakabili.

Shuhuda wa tukio hilo, mkazi wa Mtaa Nyasubi, Samweli Jushua, alisema siku ya tukio alikuwapo ndani ya benki hiyo na hakujua kinachoendelea mpaka walipoona maofisa wa benki wakikamatwa, huku akilipongeza jeshi la polisi kwa kufanyakazi kwa weledi bila kusababisha taharuki kwa wananchi.






# TADB yashika nafasi ya pili miongoni mwa Taasisi za Fedha za Maendeleo za SADC

TADB
Tanzania Agricultural Development Bank
"The Farmers' Bank"

**Mahe, Shelisheli – Juni 28, 2024:** Benki ya Maendeleo ya Kilimo ya Tanzania (TADB) imeshika nafasi ya pili miongoni mwa Taasisi za Fedha za Maendeleo (DFI) kati ya wanachama kumi na tatu (13) wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC). TADB ilishiriki katika tathmini ya Mwongozo wa Viwango vya Kimaadili na Mfumo wa Upimaji (Prudential Standard Guidelines and Rating System - PSGRS) kwa ajili ya Benki na Taasisi za Fedha za Maendeleo barani Afrika mwaka 2022. Ushindi huu ni kwa kutambua mchango wa TADB katika utawala bora, viwango vya kimaadili vya kifedha na ubora wa kiutendaji miongoni mwa Taasisi za Kifedha za Maendeleo za Afrika.

Ushindi huo ulitangazwa wakati wa mkutano wa kamati ndogo ya SADC-DFI uliofanyika Juni 28, 2024, katika Hoteli ya Savoy Seychelles huko Mahe, Shelisheli. Mkutano huu ulihitimisha Mapitio na Upimaji wa 13 wa Taasisi za Fedha za Maendeleo za Afrika, ukijumuisha tathmini ya kina ya taasisi thelathini na nne (34) barani Afrika, kumi na tatu (13) kati ya hizo zikiwa ni wanachama wa mtandao wa DFI za SADC.

Mchakato wa tathmini kwa kutumia Mwongozo wa Viwango vya Kimaadili na Mfumo wa Upimaji (PSGRS) ulijumuisha kujitathmini kwa umakini na kisha kuthibitishwa na wakaguzi wa nje kabla ya kuwasilishwa kwenye Sekretarieti ya Jumuiya ya Taasisi za Fedha za Maendeleo ya Afrika (AADFI) kwa tathmini huru, na hatimaye kupata alama kwa mujibu wa viwango vya PSGRS.

TADB ilipata alama 91% na kushika nafasi ya pili baada ya "Gapi-Sociedade de Investimentos" kutoka Msumbiji, iliyopata alama 92% miongoni mwa DFI za SADC. Washiriki wengine muhimu walijumuisha Benki ya Maendeleo ya Angola, Benki ya Akiba ya Botswana, Benki ya Maendeleo ya Namibia, Benki ya Maendeleo ya Shelisheli, Benki ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Shirika la Maendeleo ya Viwanda "South Africa", Shirika la Fedha za Maendeleo la Eswatini, Mfuko wa Maendeleo ya Usafirishaji (Malawi), Benki ya Maendeleo ya Miundombinu ya Zimbabwe, Shirika la Maendeleo ya Biashara Ndogo na za Kati (Zimbabwe), na Benki ya Maendeleo ya TIB (Tanzania).

Tathimini ya PSGRS kwa ajili ya Benki na Taasisi za Fedha za Maendeleo iliandaliwa na Jumuiya ya Taasisi za Fedha za Maendeleo ya Afrika (AADFI) kwa ushirikiano na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB). Tathmini ya PSGRS sio tu inatathmini nguvu za taasisi na maeneo yanayohitaji kuboreshwa bali pia inatumika kama kipimo muhimu kwa viwango vya kimataifa vya mikopo na kuboresha upatikanaji wa masoko ya mitaji.

Akionyesha furaha yake kuhusu nafasi ya TADB, Mkurugenzi Mtendaji Bw. Frank Nyabundege, alibainisha kuwa utawala bora, usimamizi wa kifedha wa kimkakati, pamoja na uwezeshwaji wa kifedha kutoka serikalini unaolenga kuongeza utoaji wa mikopo katika sekta ya kilimo vilikuwa ni nguzo muhimu iliyosaidia mafanikio ya TADB. Alisema, "Tunashukuru Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. TADB inaendelea kujidhatiti katika kutimiza dhamira zake kuu, ikilenga kuchagiza maendeleo ya kilimo kutoka kilimo cha kujikimu kwenda kilimo cha kibiashara pamoja na kuchangia utoshelevu na usalama wa chakula nchini Tanzania"



*Frank Nyabundege Mkurugenzi wa Benki ya Maendeleo ya kilimo ya Tanzania*

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni wakati wa wazawa kupambania namba

**WAKATI** klabu za Ligi Kuu zipo katika harakati za kufanya usajili kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano, tunaona idadi kubwa ya wachezaji wa kigeni wakisajiliwa na timu hata zile ambazo huko nyuma zilikuwa hazifanyi hivyo, sasa nazo zimeamua kushusha wachezaji kutoka nje ya nchi.

Klabu kama KMC na hata Prisons ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikiamini wazawa, zimeanza kuleta wachezaji kutoka nje, huku 'Wajelajela' hao wao wakianza hivyo tangu msimu uliopita.

Siku kadhaa nyuma nilimsikia kiongozi mmoja wa Mashujaa FC, naye akitamani kikosi hicho kiwe na wachezaji wa kigeni, ambapo alisema wanaweza kuomba kibali kwa ajili hiyo, ingawa hatuna uhakika kama wataruhusiwa.

Kwa jinsi tunavyoona ni kwamba huenda msimu ujao klabu 14 zinaweza kuwa na wachezaji wengi wa kigeni, kasoro Mashujaa FC, na JKT Tanzania tu, na si kwa sababu hazitaki, bali ni sababu za kiusalama kwani zinamilikiwa na majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama.

Klabu kama Simba, Yanga na Azam tuna uhakika zitakuwa na wachezaji 12 wanaoruhusiwa kikanuni, lakini pia Singida Black Stars na Tabora United, inawezekana ikawa hivyo hivyo.

Zilizobaki zinaweza kuwa na angalau wasiopungua watano kushuka chini. Pamoja na idadi hiyo, bado kimahesabu wachezaji wa Kitanzania watakuwa wengi kuliko wageni.

Ambacho tunashauri kwa wachezaji wa Kitanzania ni kuchukua changamoto hiyo kuwa chanya kwao kuliko hasi.

Huu ni wakati wa kufanya mazoezi kwa bidii ili kuwashawishi makocha wawapange kwa jambo ambalo litatoa nafasi kwao kuitwa kwenye Timu ya Taifa, Taifa Stars.

Hakuna kocha yeyote anayeweza kupanga kikosi chake kwa sababu ya upendeleo wa wageni au wenyeji, bali ni kwa jinsi mchezaji atakavyoonekana anachokifanya mazoezini.

Kocha hupanga yule ambaye atampa matokeo, na yupo tayari kupambania timu kwa wakati huo, haijalishi ni mgeni ama mzawa.

Kwa bahati mbaya sana baadhi ya wachezaji wa Kitanzania hawajitambui na wana tabia ya kubweteka na mafanikio kiduchu na si wapambanaji. Wengi wanapenda tu kusaidiwa na kubebwa na kanuni, na si uwezo wao uwanjani.

Baadhi yao wanaridhika na mishahara mikubwa wanayoipata haswa wanapokuwa kwenye vikosi vya Simba, Yanga na Azam, magari na starehe za muda mfupi, kiasi cha kushindwa kuonyesha viwango walivyokuwa navyo huko walikotoka kabla hawajafika timu hizo.

Matokeo yake msimu mmoja baadaye wanatokewa kwa mkopo na kuishia huko kwani imekuwa mara chache sana kurudishwa tena baada ya kutolewa kwa mkopo.


Mfano msimu uliopita kwenye kikosi cha Simba, wenye uhakika wa kupata namba walikuwa ni wanne tu, Shomari Kapombe na Mohamed Hussein 'Tshabalala', Kibu Denisi na Mzamiru Yassin, namba zingine zote zilitawaliwa na wageni.

Kwa sasa Simba ina makocha wapya ambao hawamfahamu yeyote, hivyo ni wakati wao kuchangamka, kumuonyesha walichonacho, pamoja na bidii, kujituma ili kumshawishi kupata namba kwenye kikosi cha kwanza.

Inaonekana si wachezaji wengi wa Kitanzania waliotapakaa ulimwenguni kwa ajili ya kusaka malisho kama nchi za wenzetu, na hata baadhi yao waliokuwa huko, msimu huu wamerejea nchini, kama Abdulrazack Hamza aliyerejea kutoka Afrika Kusini alipokuwa akiichezea Klabu ya Super Sports na Oscar Paul aliyejiunga na KMC, akitokea Kakamega Home Boys, hivyo kilichobaki ili kutengeneza kikosi bora zaidi cha Stars ni kung'ang'ana kufanya vizuri kwenye mazoezi, kujituma na kufuata maelelezo ya mwalimu ili kupata namba.

Tuna uhakika Mtanzania yeyote ambaye atakuwa kwenye kikosi cha kwanza katika timu yenye wachezaji wengi wa kigeni, anafaa kabisa kuichezea Taifa Stars, hivyo ni wakati sasa kwao kupambana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mfumo Kombe la Kagame sasa ubadilishwe kurudisha msisimko

Na Adam Fungamwango

**MICHUANO** ya Kombe la Afrika Mashariki na Kati, maarufu kama Kombe la Kagame inaanza kutimua vumbi kesho nchini.

Ni michuano ambayo inazishirikisha klabu bingwa za nchi au zinazoteuliwa kutoka Ukanda wa CECAFA. Mwaka huu linajulikana kama , Dar Port Kagame Cup, ikizishirikisha jumla ya timu 12.

Mara ya mwisho ilifanyika hapa hapa nchini miaka mitatu iliyopita, ambapo Express ya Uganda ilitwaa ubingwa kwa kuifunga Nyasa Big Bullets bao 1-0 katika mechi ya fainali.

Tangu 2021 michuano hiyo haijafanyika na inavyoonekana ni kwa sababu ya kukosa wadhamini.

Hata hivyo, binafsi naona kuwa wadhamini hawawezi kujitokeza tu hivi hivi bila kwanza michuano kuonekane inavutia watu.

Wala simung'unyi maneno kuwa michuamo ya Kombe la Afrika Mashariki na Kati, maarufu kama Kombe la Kagame miaka hii ya karibuni imepoteza mvuto na msisimko.

Haipo kama zamani ambapo wiki chache kabla, tayari mashabiki wa soka Ukanda wa Afrika Mashariki wanakuwa na kimuhemuhe cha kutaka kujua nini kinafanyika au kinaendelea.

Nakumbuka miaka ya 1980 hadi mwishoni mwa 1990, ilikuwa ni moja kati ya makombe makubwa mno, yenye mvuto na msisimko wa hali ya juu.

Ni michuano ambayo ilizivutia mpaka timu za Ukanda wa Kusini mwa Afrika ambazo zilikuwa zikishiriki na kuleta hamasa kubwa.

Kulikuwa na timu kali na tishio miaka hiyo kama vile Admarc Tigers. Limbe Leaf na Bata Bullets za Malawi, State House Tornados ya Zimbabwe, Mufulira Wanderers ya Zambia na zingine nyingi ambazo zilikuwa maarufu na kujulikana na mashabiki wengi wa soka kutokana na ukali ya vikosi hivyo.

Zilichanganyika na klabu za Al Hilal na El Merrikh za Sudan, SC Villa ya Uganda, AFC Leopards na Gor Mahia za Kenya, wakati huo zikiwa za moto sana.

Ilikuwa patashika kila nchi ambayo michuano hiyo inachezwa, huku Tanzania zikiwakilishwa zaidi na Klabu za Simba na Yanga, Zanzibar timu ambazo zilikuwa zikicheza sana ni Small Simba, Miembeni, KMKM na zinginezo.

Kila shabiki wa soka anaweza akawa anajiuliza kwa nini michuano hiyo imeonekana kukosa msisimko?

Ninavyoona mimi ni kwamba viongozi wa CECAFA wanashindwa kuumiza vichwa ili kuifanya michuano hiyo kwenda na wakati.

Wakati viongozi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), wakionekana mara kwa mara kufanya mabadiliko ili kuboresha michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, wa CECAFA bado wamelala.

Kama CAF wangekuwa na mawazo mgando hadi leo michuano yao ingekuwa ya mtoano kuanzia mwanzo hadi mwisho kama zamani.

Na hata walipobuni makundi na kuanza na timu nane, baadaye walikaa na kuona waongeze timu. Hawa ndiyo wanaonekana kwenda na wakati, huku CECAFA, michuano mikongwe kabisa ikionekana kufifia.

Ndiyo maana utaona hata Klabu za Simba, Yanga na Azam ambazo huenda zingenogesha, zimejiondoa. Huwezi kuweka michuano kipindi cha 'pre season', ambapo wachezaji ndiyo kwanza wanajikusanya kutoka mapumziko.

Umefika wakati sasa viongozi wa CECAFA kuangalia muda sahihi wa kuendesha michuano hiyo, lakini hata kubadilisha mfumo.

Ingeweza kuchezwa hata kwa mtindo wa ligi, nyumbani na ugenini, hadi kufikia timu kuingia robo, nusu fainali na fainali, ambapo ingeendeshwa kwa msimu mzima.

Ni suala la CECAFA kuwasiliana na mashirikisho yale ya Afrika Mashariki kuweka kalenda zao za ligi vizuri tu ili kufanyika kwa michuano hiyo.

Nadhani ingeleta mvuto, na vile vile kupata wadhamini wengi kwani hakuna kampuni ambayo haitaki matangazo yake yaonekane msimu mzima.

## HABARI KITAIFA

# Zaidi wananchi 400,000 wafikiwa msaada kisheria

**Na Elizabeth Zaya**

WANANCHI 490,000 wa mikoa saba wamefikiwa na Kampeni ya msaada wa kisheria iliyopewa jina la 'Mama Samia Legal Aid Campaign' kwa kutatuliwa migogoro ikiwamo ya ardhi.

Kaimu Mkrugenzi wa Huduma za Msaada wa Kisheria kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Ester Msambazi, aliiambia Nipashe katika banda la Mama Samia Legal Aid Campaign kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaama (DITF) yanayoendelea Barabara ya Kilwa, wilayani Temeke.

Alisema baadhi ya migogoro iliyotatuliwa kupitia kampeni hiyo ni inayohusu ushauri wa msaada wa kisheria, kuelimishwa kwa suala lolote la kisheria wanapohitaji kuwasilisha mahakamani, kuwaunganisha na mawakili, kuandaliwa nyaraka na huduma nyinginezo zinazohitaji kutatuliwa kisheria.

"Wizara iliona umuhimu wa kuleta kampeni hii ya kitaifa ya msaada wa kisheria ambayo imepewa jina Mama Samia Legal Aid Campaign katika maonesho haya ya Sabasaba kutokana na umuhimu wake katika kutatua migogoro ya wananchi na kampeni hii inatolewa bure," alisema Ester ambaye pia ni Msajili wa Mashirika yanayotoa huduma za msaada wa kisheria.

"Tuko hapa kuungana na wadau wengine, kuhakikisha mwananchi hakosi huduma yoyote ya kisheria akiwa katika viwanja hivi vya Sabasaba, kama kuna mtu ana jambo lake linamtatiza na anataka litatuliwe kisheria atumie fursa hii ya maonesho, tuko mpaka mwisho kuhakikisha tunawafikia wananchi wengi zaidi."

Aidha, alisema kesi ambazo wakili anaweza kumsaidia mwananchi baada ya kufika katika kampeni hiyo ya kitaifa ni pamoja na hati za kufungua mashauri mahakamani iwe ni kufungua kuomba usimamizi wa mirathi, masuala ya madai, matunzo ya watoto, kuasili watoto na masuala mengine ya kisheria ambayo nyaraka zake zinapelekwa mahakamani.

Kwa mujibu wa Ester, ipo mikataba mtu anaweza kusaidiwa kuandika pamoja na huduma nyingine ambazo mwananchi wa kawaida hawezi kwenda kuzipata kutokana na kutokuwa na uwezo wa kumlipa wakili.

Pia, alisema tangu kuanza kwa maonesho ya Sabasaba Juni 28, mwaka huu, mwitikio wa wananchi kuomba msaada wa kisheria hasa kwenye migogoro ya ardhi umekuwa mkubwa, na wengi wamekutanishwa na wataalam wakasaidiwa.

"Wananchi waliojitokeza ni wengi tangu tumefika hapa Juni 28 na hii inatuonyesha kwamba huduma zetu zimefika mbali sana na wananchi wamepata taarifa," alisema Ester.

Mama Samia Legal Aid Campain ilianza kutekelezwa mwaka jana Aprili mkoani wa Dodoma na mpaka sasa mikoa saba imefikiwa.

Mikoa mingine iliyofikiwa ni Manyara, Singida, Simiyu, Shinyanga , Njombe na Ruvuma.




Makamu wa Rais wa EIB,Thomas Ostros (wa tano kutoka kulia), Mkurugenzi wa Biashara wa Kanda ya Afrika Mashariki na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya KCB Tanzania, Cosmas Kimario (wa tatu kutoka kulia), pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Matibabu cha Regency, Lalit Kanabar (wa nne kutoka kulia) walipotembelea Kituo cha Matibabu cha Regency wiki iliyopita.**PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Tume Atomiki: Tumieni kwa usahihi maji ya visima

**Na Pilly Kigome**

TUME ya Nguvu ya Atomiki Tanzania (TAEC) imewataka Watanzania kujali afya zao kwa kufanya matumizi sahihi ya maji ili kuepuka magonjwa yatokanayo na mionzi itokayo chini ya ardhi.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kutoka Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC), Peter Ngamiro wakati akizungumza na vyombo vya habari katika Maonesho ya 48 ya Sabasaba yanayoendelea, jijini Dar es Salaam.

Alisema wananchi wanatakiwa kuwa makini na matumizi sahihi ya maji hasa ya visima kwa kuyapima kuepuka yenye asili ya mionzi kwenye udongo na mazingira kama madini ya urani.

Ngamiro alisema Tume hiyo imeshaanza utaratibu maalum wa kupita majumbani na viwandani kupima maji, ili kuwalinda walaji kama yako salama kwa matumizi ya binadamu au la.

Aidha, aliwataka Watanzania kuonesha ushirikiano wanapofikiwa ikiwamo kupeleka sampuli ya maji kupimwa, kwa ajili ya kuhakiki ili kulinda afya zao.

Tume hiyo pia ina majukumu matatu ikiwamo kudhibiti na kusimamia matumizi salama ya mionzi, ili kulinda wananchi wagonjwa na wafanyakazi dhidi ya matumizi ya mionzi.

Peter aliwahamasisha wananchi kufanya matumizi sahihi ya teknolojia ya mionzi au nyuklia katika sekta za afya, kilimo, viwanda, nishati, migodi na ujenzi.


Jukumu la tatu ni kufanya utafiti kuishauri serikali kuhusu mikataba mbalimbali inayohusu nyuklia na kufanya ukaguzi.

"Tunawakaribisha wananchi wote wa Jiji la Dar es Salaam na viunga vyake kufika katika banda letu waweze kujifunza na kupata elimu na uelewa na kazi zinazofanywa na tume," alisema.

Ofisa Utafiti kutoka TAEC, Lazaro Meza, alisema upimaji huo wa maji umetokana na Sheria ya Nguvu za Atomu ya mwaka 2003 No.7 ya upimaji wa sampuli ya vyakula baada ya kufanyiwa mapitio sasa imekuja kupima vyakula pamoja na maji kwa kuwa ni sehemu ya mapishi.

Alisema maji ni kiungo muhimu yakipata uchafuzi wa mionzi chakula kitakuwa tayari kimepata madhara itokanayo na mionzi hiyo.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# Bank of India (Tanzania) Ltd.

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

*Relationships beyond banking*

## ISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019

### MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

**Service Charges (Exclusive of VAT and Government Levy on DigitalTransactions) (The applicable VAT (Value added Tax) and Govt Levy on digital Transaction to be collected during the collection of service charges)**

### A. REMITTANCE –OUTWARD

| Sr. No. | Item | Charge in TZS or Equivalent to TZS |
|---|---|---|
| **TISS Remittance** (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | Remittance -TZS or TZS Equivalent Transaction value | |
| | Between TZS 1 to 10 million | 2,000 |
| | Between TZS 10 million to 50 million | 5,000 |
| | Above TZS 50 million | 10,000 |
| | | |
| **TIPS AND TACH** | Transaction value | |
| | Between TZS 1-TZS 50,000 | 500 |
| | Between TZS 50,001-TZS 500,000 | 1,000 |
| | Between. TZS 500,001- 5,000,000 | 1,500 |
| | Between. TZS 5,000,001- 20,000,000 | 2,500 |
| | | |
| **Other Outward Remittance** | 1USD up to 6,000 | USD 15 |
| | USD 6,001 – 10,000 | USD 30 |
| | Above USD10,000 | @ 0.35% Maximum USD 75 |
| Tracer Charges | Irrespective of Amount | USD 30 |
| Recall back funds charges | Irrespective of Amount | USD 30 |

### B. REMITTANCE –INWARD

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | From inside Tanzania (TISS, TIPS AND TACH) | Free |
| | From outside Tanzania: as under | |
| | For Current /Overdraft Accounts | 0.35% of inwards remittance Minimum USD 18 Maximum USD 70. |
| | For Saving Accounts | |
| | USD 0 up to USD 100 | Free |
| | USD 101 up to USD 500 | USD 10 |
| | Above USD 500 | USD 18 |

### C. DEPOSIT AND RELATED SERVICES

| Item | TZS A/c | USD A/c |
|---|---|---|
| **Saving Account :-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 2000 |
| Cash withdrawal charges over USD 2,000 to USD 5000 per day | -- | 0.25% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25 Mn per day | 0.10% of withdrawal amount | |
| Cash Deposit charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of deposited amount |
| Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both for below and above USD 5,000) | -- | 12% (Min USD 1) of the aggregate small currency amount |
| **Current Account:-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 5000 |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of withdrawal amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | 0.15% of withdrawal amount | -- |
| Cash deposit charges over USD 10,000 per day | | 0.60% of deposit |
| **Maintenance of minimum balance: -** | | |
| For Saving Account-Without Cheque Book Facility | TZS 50,000 | USD 50 |
| With Cheque Book Facility | TZS 200,000 | USD 200 |
| For Current Account | TZS 200,000 | USD 200 |
| **Minimum balance charges (in case of non-maintenance of minimum balance)** | | |
| Saving Account - Without cheque book | TZS 900 p.m | USD 4 p.m |
| With cheque book | TZS 3600 pm | USD 15 p.m |
| Current Account- | TZS 20,000 p.m | USD 15 p.m |

### D. Other Common Charges

| Item | Charges | |
|---|---|---|
| | **TZS A/c** | **USD A/c** |
| Stop Payment Instructions | TZS 35,000 | USD 28 |
| Regular statement of a/c (Monthly) | Free | Free |
| Interim/additional statement | TZS 1500 per page | USD 1.50 per page |
| Issue of bankers' cheque | TZS 40,000 | USD 30 |
| Cancellation of bankers cheque/DD | TZS 20,000 | USD 15 |
| Issue of Duplicate Bankers cheque/Demand Draft/ Duplicate FDR | TZS 30,000 | USD 20 |
| Application charge for Treasury Bond | TZS 100,000 | USD Equivalent to TZS 100,000 |
| Issue of Balance certificate (Saving Account) | TZS 20,000 | USD Equivalent to TZS 20,000 |
| Issue of Balance certificate (Current Account) | TZS 50,000 | USD Equivalent to TZS 50,000 |
| Signature verification and Photo Attestation charges for Domestic A/c Holders | TZS 10,000 | USD Equivalent to TZS 10,000 |
| Verification of Documents such as KYC Documents along with verification of Photo and Signature of Customer Mentioned account with Bank of India- in India /Overseas | TZS 25,000 | USD Equivalent to TZS 25,000 |
| Savings bank customer Identification card-One time | TZS 20,000 | USD 10 |
| Dormant a/c Activation Per Activation Fees | Individual TZS 5,000 Corporate TZS 12,000 | Individual USD 3 Corporate USD 6 |
| Account Freezing/un freezing Charges | Free | Free |
| SMS Alert facility | Free | Free |
| Email Alert Facility | Free | Free |
| Monthly Statement on Registered Email | Free | Free |
| Balance Inquiry (Over the Counter) | Free | Free |
| Charges for Deletion of Decease Person Name from the Saving Account | Free | Free |
| Charges for Addition/modification Account such as Change in respect of Corporate A/c | TZS 20,000 | USD 10 |
| Updating of Mobile No. in A/c (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Change /Modification in Address (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Issuance of No Dues Certificate for Non-Borrowers. | TZS 10,000 | USD 7 |
| Ledger Folio Charges per Folio (40 lines per Folio) only for Current and Overdraft Accounts | TZS 6,000 per Folio | USD 4 per Folio |
| Postages/Courier Charges Inland/Foreign | TZS 30,000 or actual charges whichever is higher | USD Equivalent to TZS 30,000 |

### E. CLEARING SERVICES

| Item | Charge/Fees | |
|---|---|---|
| | **TZS A/c** | **USD A/c** |
| Within walking distance-1 km | TZS 70,000 | USD 45 |
| Far off distance –more than 1 km | TZS 95,000 | USD 65 |
| Cheque returned charges –financial reasons (inward/outward) | TZS 70,000 | USD 55 |
| Inward/outward cheque collection -USD | 0.60% Min comm.18 postages 90 | 0.60% Min comm.18 postages 90 |

### CREDIT MATTERS

| Charge/Fees | |
|---|---|
| | |
| **Proposal Processing Charges: -** | |
| New Overdraft/Term Loan/Demand Loan | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) |
| TOD/TOL/ADHOC | Proportionate to 1.50% for TOL/TOD/ADHOC Period minimum USD 60 |
| New NFB BG/LC Facility | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) |
| Review of Overdraft Limit | 1.50% on entire sanctioned amount. |
| Review of Term Loan Demand Loan Personal Loan Vehicle Loan Loan Against Property Etc. | 0.15% maximum USD 600 or TZS 1.20Mn on the reviewed amount and 1.50% on the additional Term Loan /Demand Loan amount. |
| Schematic Lending up to 36 months/Staff Loan | Nil |
| Prepayment charges | 2.50% of the prepaid loan amount. |
| Documentation charges for New Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan/Non Fund base Limit | Actuals as per advocate Bill + 0.30% handling charges |
| | 1) No Documents charges would be applicable for TOD/TOL/ADHOC Limit, however actual expenses if any to be recovered.<br>2) Documentation charges also NOT Recoverable for the Loan/Overdraft against FDR. |
| Charges for Amendments/Modification of Sanction Terms | 0.25% on the sanctioned limit |
| | **We enumerate the illustrative instances of Modification in Terms and Conditions to be effected at the request of the Borrower where this charge will be levied: -**<br>1) Substitution of Collateral Securities/Personal Guarantee<br>2) Release of Personal Guarantee/Collateral Security.<br>3) Interchangeability of limits.<br>4) Change in project/items of Machinery<br>5) Ceding of charges on assets(Pari-Passu)<br>6) Restructuring, Rephasement of Loans/ Deferment of Loan installments.<br>7) Approvals for mergers & amalgamations.<br>8) Any other miscellaneous credit related approvals. |
| Revalidation of Sanction | **25% of Applicable PPC Charges on Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan** |
| Lead bank Charges | **USD 1000 or equivalent in TZS per annum/one time** |
| Fee for Opening Escrow/TRA A/cs (Trust and Retention A/cs) | **Where**<br>**We are Lead bank: Nil**<br><br>**We are Not Lead Bank:**<br>USD 500 or equivalent in TZS per annum/one time |
| Charges for Supplying copies of Loaning Documents to Customer. | First instance: Free<br>**USD 10 or equivalent in TZS for further requirement.** |
| Non/Delayed Submission of Audited Financial Statements of the Company OR wherever applicable | **USD 100 or equivalent in TZS per month or part thereof** |
| | **Note:-**Audited Financial statements of the firm/company within 6 months from closure of Financial Year or as approved by TRA for the relevant year. |
| Inspection charge | **TZS 50,000** or equivalent to USD per visit /inspection or at least once in quarter whichever is higher. |
| | **Note:-**<br>1) Out of Pocket Expenses to be recovered additionally along with regular inspection charges wherever applicable<br>**2) Project Monitoring Inspection Charges/Technical Due Diligence Inspection charges:** Considering the fact that this inspection is proposed for safeguarding banks Interest, normal inspection charges besides travelling, boarding/lodging expenses are to be recovered from the borrower. |
| Issuance of No objection certificate (NOC) | **USD 100 or equivalent in TZS** |
| 1st party/3rd party Overdraft/Loan against deposit of our Bank (BOITL) | Waiver of Processing & Documentation charge. |
| Overdraft/Term Loan/Demand Loan Conversion Charges (Currency Conversion) | For Overdraft account 0.50% of Sanction Limit.<br>For Term Loan/Demand Loan 0.50% of O/s Amount |
| Earmarking of Limits | **USD 500 or equivalent in TZS per annum** |
| Non Compliance of Sanction terms/Commitment charges | **1.00% additional Penal Interest to be charge till compliance of Sanction terms** |

| **D&B/ Other Credit Information Search for per Borrowal a/c (New/Additional/Review of limit)** | | |
|---|---|---|
| Up to TZS 20 Mn/USD 10,000 (Only for new and additional Limit. **Review – No charge**) | USD Facility<br>USD 5 | TZS Facility<br>TZS 5,000 |
| Over USD 10,000 to USD 50,000/ Over TZS 20 Mn up to TZS 100 Mn | USD 10 | TZS 20,000 |
| Over USD 50,000/TZS 100 Mn | USD 50 | TZS 100,000 |
| D&B Search for non-Borrower, on request | USD 50 | TZS 100,000 |
| Charges for Furnishing copy of Credit Information report obtained from CIC | **TZS 20,000** | **USD 10** |

| **Guarantee (Performance/Financial) :-** | |
|---|---|
| Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part thereof minimum for one quarter. |
| Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate |
| Swift Charges | **As Applicable** |
| Postages | **As Applicable** |
| Revert of Guarantee before Expiry | **Minimum 1 Qtr BG Commission to be recovered for part of quantum of full guarantee commission to be recovered** |
| Closure of Guarantee After Expiry of Claim Period | Nil |
| Invoke of Guarantee | **USD 200 or equivalent in TZS** |
| | **A. Financial Guarantees: -**<br>1. In favour of Customs/Excise/Tax Authorities towards tax/Duties payment Etc.<br>2. Favouring Courts for Release of Amounts.<br>3. For Guaranteeing Loan payments.<br><br>**B. Performance Guarantees: -**<br>1. In lieu of earnest money deposit<br>2. In lieu of tender deposit<br>3. In lieu of security deposit<br>4. To obtain advance payments (generally exports)<br>5. To obtain mobilization advance (generally domestic)<br>6. Towards Direct/indirect taxes to govt. in respect of specific transaction.<br>7. For Direct/indirect taxes disputes with tax Authorities.<br>8. For payment for supplies/services made /rendered<br>9. For Securing retention amount<br>10. For Bidding/tendering for Project Contacts<br>11. For Performance in terms of any agreed contact.<br><br>**Note: - No processing charges or documentation charges are to be levied in case of Casual BG limits issued against 100% or more cash margin.** |
| **Imports :-** | |
| LC Opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| Against 100% cash margin | 50% concession on the above rate i.e. 0.67% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| LC Amendment Charges | Per amendment 0.40% of LC amount (minimum USD 60 and Maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (Same for LC against 100% cash margin) |
| Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 180 |
| Retirement of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 360 |
| Inward Bills for Collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 |
| **Exports:-** | |
| Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount Minimum USD30 Maximum USD 360 |
| Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30/- |
| LC Advising Charges | USD 150 |
| Export Bills for Collection | 0.60% of Bill amount Minimum USD 30 Max USD 360. |
| Charges for Certifying invoices subsequent to negotiation | **USD 10 Per Invoice** |
| Clean payment Received under LC | **USD 100 per occasion** |
| Advice of transfer in transferable LC | **USD 100 per advice of transfer and acceptance commission at 0.30% Minimum USD 100** |

### OTHER DISCLOSURES
### (VIAMBATANISHI NYINGINEZO)

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| 1.0 | **Base or Prime Lending rate** | 7.50% p.a. | 14.50% p.a. |
| 2.0 | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 3.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| 4.0 | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | **Up to USD 10,000** | **Up to TZS 10,000,000** |
| | 6 months | 3.00% | 6.25% |
| | Over 6 months | 3.50% | 7.25% |
| | | **Over USD 10,000** | **Over TZS 10,000,000** |
| | 6 months | 3.50% | 6.75% |
| | Over 6 months | 4.00% | 7.75% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |
| | | | |

**No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the Period covered by the Disclosure**

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 04.07.2024 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 04.07.2024 |
| 3. | Robert Kibona | General Manager | Signed | 04.07.2024 |





# Wakulima tumbaku walioathiriwa na mvua za Elnino walipwa bil.13/-

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe amesema serikali imetoa fidia ya Sh. bilioni 13 kwa wakulima wa tumbaku ambao mazao yao yaliathiriwa na mvua za Elnino msimu wa mwaka 2023/24.

Amesema pesa hizo zitapelekwa kwa wakulima kwenye akaunti zao baada ya vyama vya ushirika kuwasilisha majina ya wakulima hao kwenye vyombo vya fedha.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye sherehe za maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani ambayo kitaifa yamefanyika kwenye viwanja vya Nanenane, mkoani Tabora.

Aidha, alisema kuanzia mwaka huu, serikali itatoa ruzuku kwa wakulima wa zao hilo kwa kutenga Sh. bilioni 13.3 kwa ajili ya kununulia mbolea kwenye msimu wa mwaka 2024/2025.

Bashe alisema sekta ndogo ya tumbaku imezidi kukua na kuongezeka mwaka hadi mwaka, kwamba mwaka 2022/21 tani 60,000 zilizalishwa, mwaka 2022/23 tani 120,000.

Hivyo, alitoa agizo kwamba kuanzia sasa mikataba ya kilimo kati ya wanunuzi na wakulima itakuwa ya miaka mitatu badala ya mwaka mmoja, huku kila mwaka wawili hao watakuwa wakijadiliana kuhusu bei ya mwaka mmoja hadi mwingine.

Wakati wa maadhimisho hayo, Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko alikabidhi kompyuta tano zilizotolewa na kampuni ya tumbaku ya Alliance One, kwenda kwa vyama vya msingi vya wakulima wa zao hilo vilivyofanya vizuri kwenye msimu wa mwaka huu.

Kompyuta hizo za Sh. milioni 26 zimekabidhiwa kwa vyama vya msingi, baada ya kuibuka washindi kati ya vyama 115 ambavyo vina mikataba na kampuni hiyo nchini.

Akizungumza wakati akikabidhi vifaa hivyo, Dk. Biteko aliwaasa wakulima wa tumbaku nchini kuanza utaratibu wa kukatia bima mazao yao, ili waweze kupata fidia pale wanapofikwa na majanga kama vile ya Elnino ambayo yamewakumba msimu huu.

Msemaji wa kampuni hiyo, Wakili John Magoti, alisema zawadi hizo ni motisha kwa vyama vya msingi vya wakulima wa tumbaku vilivyofanya vizuri.

Alivitaja vigezo vilivyotumika ni kufanya malipo kwa wanachama wao kwa wakati, kufikia au kuvuka malengo ya makisio ya uzalishaji wa zao pamoja na utunzaji bora wa kumbukumbu ya mahesabu ya chama husika.

Alisema mpango wa kutoa zawadi utasaidia kupunguza kama siyo kuondosha kabisa upotevu wa nyaraka muhimu za vyama hivyo.

Vyama vilivyopata kompyuta hizo ni Ilolangulu kutoka Uyui, Igwisi kutoka Kaliua na Unyanyembe kutoka Sikonge, vyote hivi vya Mkoa wa Tabora.

Vingine ni Kikubhagulu kutoka Uvinza, Tembo kutoka Ushetu, wilayani Kahama mkoani Shinyanga.



Meneja wa Kanda ya Magharibi wa Benki ya CRDB, Jumanne Wagana (kulia) akipokea tuzo ya udhamini kutoka kwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kushoto) kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani, Ipuli mkoani Tabora kuanzia Juni 29 mpaka Julai 6, j **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

## Binti asimulia ndoa ya utoto ilivyokatisha ndoto yake

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKAZI wa wilayani Butiama mkoani Mara, Queen Maige (21) ameeleza namna alivyokatisha masomo yake baada ya kuozeshwa kwa nguvu kwa mahari ya ng'ombe sita na kukatisha ndoto yake ya kuwa askari.

Queen ni miongoni mwa wasichana 164 waliofadhiliwa mafunzo katika Chuo cha Ufundi Mwakata (SFS), chini ya udhamini wa Shirika la Wanawake katika Shirika la Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF) mkoani Shinyanga.

Alibainisha hayo juzi kwenye mahafali ya 21 ya chuo hicho ambapo wanafunzi 301 walihitimu fani mbalimbali, huku kati yake 164 wakiwa ni mabinti waliokatisha masomo yao kwa sababu mbalimbali ikiwemo ndoa na mimba za utotoni.

Alisema alihitimu elimu ya msingi mwaka 2015 katika Shule ya Msingi Kinyalili Butiama na mwaka uliofuata akiwa na miaka 15 mjomba wake alimlazimisha kuolewa kwa mahari hiyo ya ng'ombe.

Queen alisema ndoto yake ilikuwa ni kuwa askari lakini imefifia baada ya kukatishwa masomo na kuangukia kwenye ujuzi wa fundi cherehani.

Mratibu wa mradi wa Chaguo langu Haki yangu kutoka Wildaf, Joyce Kessy alisema kati ya binti hao, 45 wanatoka Musoma mkoani Mara, Kishapu (75) na Kahama (44).

Mkuu wa chuo hicho, Padri John Denisi alisema wanafunzi hao wamejifunza ufundi umeme, ushonaji, magari, bomba, sekretari, kompyuta pamoja na saluni na mapambo ujuzi utakaowasaidia kuendesha maisha yao.

Ofisa Ustawi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Swaiba Chemchem aliahidi kuwaunganisha mabinti hao katika vikundi vya ujasiriamali kwa lengo la kupata mikopo ya asilimia 10 ili kujiendeleza na kuinua kipato chao.

# Biteko apongeza CRDB kuanzisha benki ya ushirika kuchangia uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko ameipongeza Benki ya CRDB kwa kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kuanzisha Benki ya Ushirika Tanzania ili itoe huduma kwa wanaushirika na wananchi wengine ili kuchangia zaidi katika uchumi.

"Benki ya CRDB mmetoa mchango mkubwa. Nawapongeza sana. Naamini benki hii mpya itasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto za mtaji wanazokabiliana nazo wakulima na wanaushirika kwa ujumla," alisema.

Alitoa pongezi hizo kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Ipuli, mjini Tabora.

Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Abdumajid Nsekela, alisema mpaka sasa, TCDC yenye takribani miaka miwili tangu ilipoanza kutekeleza majukumu yake, imesimamia uanzishaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika na hatua zinazoendelea ni ufuatiliaji wa leseni kutoka BoT ili ianze kufanya kazi ndani ya mwaka huu.

"Tulijiwekea lengo la kukusanya Sh. bilioni 20 ili kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika na mpaka sasa tuna zaidi ya Sh. bilioni 18 zinazotosha kukamilisha mchakato huu. Benki ya CRDB imewekeza zaidi ya shilingi bilioni 10 kwenye mtaji huu," alisema Nsekela akibainisha kuwa ushirika sasa unaendeshwa kidijitali kwa kuwa mpaka Juni 2024 vyama 6,361 vya ushirika vyenye wanachama 1,604,224 vilikuwa vinatumia mfumo huo.

Maboresho yaliyofanyika, yameviwezesha vyama vya ushirika kujiendesha kibiashara kwa kufufua viwanda na kujenga vipya ili kuongeza thamani ya mazao ya wakulima, kuhamasisha ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum mfano mifugo, uvuvi na madini pamoja na kuimarisha uwekezaji wa mali za ushirika. "Tume iliratibu utambuzi wa mali za vyama vikuu vya ushirika na SACCOS daraja B. Jumla ya mali za vyama vya ushirika 610 zenye thamani ya Sh. trilioni 4.2 zimetambuliwa," alisema.

Akitoa salamu, Meneja wa Kanda ya Magharibi ya Benki ya CRDB, Jumanne Wagana, alisema ili kufanikisha kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika, wametoa Sh. bilioni 10.2 pamoja na wataalam wa kusimamia uendeshaji wa taasisi muhimu za ushirika. "Benki ya CRDB ilitoa Sh. bilioni 3.2 kwa Benki ya Wananchi Tandahimba (TACOBA) na shilingi bilioni saba kwa Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) pamoja na wataalamu wanaosaidia kwenye shughuli za uendeshaji wa taasisi hizi zikiwa ni juhudi za kufufua ushirika nchini na kuziwezesha zijiendeshe kwa faida na tija zaidi," alisema Wagana.

"Uwekezaji huu ndio unaochagiza kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika. Bodi ya wakurugenzi, menejimenti na wafanyakazi wa Benki ya CRDB tunajivunia mafanikio haya ambayo kwa miaka ijayo, yatakuwa na mchango mkubwa kwenye kipato cha mwanaushirika mmojammoja na kuimarisha uchumi wa kaya na taifa kwa ujumla."

Vilevile, Wagana alisema Benki ya CRDB inawawezesha wakulima kupata pembejeo za kilimo, kulima na kuongeza uhakika wa mavuno pamoja na kuwaunganisha na wanunuzi wa mazao yao kutoka ndani na nje ya nchi.

"Hadi Juni, Benki ya CRDB imetoa mikopo yenye thamani ya Sh. trilioni 1.81 sawa na asilimia 43 ya mikopo yote itolewayo na benki kwenye sekta ya kilimo nchini. Kati ya mikopo hiyo tuliyoitoa, Sh. bilioni 944.6 zimeelekezwa kwa wakulima wadogo ambao ni wanachama wa vyama vya ushirika (AMCOS) zipatazo 541 ili kuongeza tija kwenye uzalishaji kwa kununua pembejeo za kisasa, kujenga maghala, kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao, miradi ya ufugaji, na uwekezaji kwenye misitu, uvuvi na biashara," alisema Wagana.

Maonesho ya Siku ya Ushirika Duniani yalifunguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan Juni 29 na kuhitimishwa Julai 5 na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko.

Nipashe Spotika




KLABU 4 ZA LIGI KUU ENGLAND ZINAZOHITAJIKA SAINI YA COSTA UK. 12-13



NICO WILLIAMS

# NYOTA WA EURO WANAOPASWA KUSAJILIWA EPL

**LONDON,** England

MOJA ya jambo kubwa katika soka la kimataifa; mchezaji anayefanya vema kwenye mashindano makubwa anakuwa na uwezekano wa kusonga mbele zaidi.

Mfikirie Enzo Fernandez baada ya Kombe la Dunia la Qatar 2022. Jack Grealish baada ya Euro 2020. Au mfano bora kabisa - Karel Poborsky baada ya Euro 1996.

Kwa hiyo ni nani anapaswa kusajiliwa kutoka mashindano ya Euro 2024 msimu huu huko Ujerumani?

### Nico Williams (Athletic Bilbao)

Mshambuliaji wa Athletic Bilbao mwenye umri wa miaka 21, amecheza zaidi ya mechi 120 dhidi ya klabu kubwa, winga huyo amefanya vema kwenye michuano ya Euro 2024 hadi sasa.

Alifunga bao zuri dhidi ya Georgia, na kudhihirisha kipaji chake. Anaweza kuwa mmoja wa wachezaji wa Ulaya wanaohitajika sana baada ya michuano hiyo.

Williams anafaa kucheza mbele chini ya kocha Arne Slot pale Liverpool. Ana kasi, mwepesi, analiona goli na ana ujasiri wa ujana. Mohamed Salah anaweza kuondoka kwenye timu hii mwaka ujao na dogo huyu anaweza kuvaa viatu vyake.

Pia anaweza kutua Manchester United ambako kwa kushirikiana na mawinga wa sasa anaweza kufaa na anaweza kucheza pande zote mbili. Yeye upande wa kulia na Alejandro Garnacho kushoto, itakuwa safi kabisa.

### Christoph Baumgartner (RB Leipzig)

Baumgartner amesaidia kupatikana mabao tisa katika michezo yake tisa iliyopita akiwa na Austria (mabao sita na pasi za mwisho tatu).

Mchezaji wa timu ya Austria chini ya kocha Ralf Rangnick. Ni mchezaji wa Klabu ya RB Leipzig. Baumgartner ni kiungo mkabaji mwenye umri wa miaka 24, mwenye jicho la kulenga lango.

Alishinda dhidi ya Poland na kutengeneza bao la ushindi la Marcel Sabitzer dhidi ya Uholanzi katika mchezo wa mwisho wa kundi na kuisaidia Austria kuongoza Kundi C juu ya Ufaransa.

Anaonekana ni mchezaji mzuri lakini pia ni mtukutu katika mtindo na ustadi wake.

### Riccardo Calafiori (Bologna)

Italia daima imekuwa ikizalisha walinzi wazuri, Calafiori mwenye umri wa miaka 22, anaweza kuwa mlinzi mwingine bora. Anafanana na gwiji wa miaka ya 2000, Alessandro Nesta.

Calafiori alitajwa katika kikosi cha Kocha Mkuu Luciano Spalletti kilichoshiriki Euro 2024, Calafiori alikuwa muhimu sana. Alikosa mechi ya hatua ya 16-bora dhidi ya Sweden na Italia ikatolewa.

Calafiori anaweza kuleta usaidizi mzuri kwa Gabriel ikiwa atasajiliwa Arsenal inayotajwa kumuwania.

Calafiori bado ni mdogo, lakini tayari ana uzoefu wa kutosha na anaweza kuimarisha safu ya nyuma.

Ni mchezaji wa kati ambaye anajua kucheza mpira na ana ustadi. Ni mzuri sana.

### Georges Mikautadze (Metz)

Katika mshangao wa wengi wa ushindi wa Georgia dhidi ya Ureno, Mikautadze alifunga katika kila mechi kati ya mechi zao tatu za kundi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, pia alifanikiwa kufunga mabao 13 katika mechi 20 za Ligue 1 akiwa na Klabu ya Metz msimu uliopita licha ya kushuka daraja.

Mikautadze utakuwa usajili mzuri kutokana na jinsi anavyocheza vizuri. Bila shaka Mikautadze ni mchezaji bora kutoka ligi ya chini ya Ufaransa, kama Riyad Mahrez.

NI mwepesi, kijana na anajua kutupia katika wavu.

### Giorgi Mamadashvili (Valencia)

Mchezaji mwingine wa timu ya Georgia, kipa Mamadashvili amekuwa bora nchini Ujerumani.

Ana umri wa miaka 23, alionesha uwezo mkubwa katika mchezo wa pili wa kundi dhidi ya Jamhuri ya Czech, akiokoa mara 11 ili kujihakikishia pointi muhimu. Ikiwa timu za Ligi Kuu England zinatafuta kwa dhati namba moja mpya wa muda mrefu, Mamadashvili anafaa.

Dirisha zuri la uhamisho litajumuisha kusajili golikipa. Mamadashvili amevutia sana kwa kuokoa vizuri na itakuwa bora kusajiliwa.

Mamadashvili amekuwa kipa mzuri katika goli la Georgia, huku Gavin Bazunu akiwa nje kwa muda mrefu, anaweza kuwa golikipa bora zaidi baadaye.

## ISIKUPITE

CRISTIANO Ronaldo ameshindwa kufunga hata bao moja katika mashuti 23 aliyopiga langoni kwenye michuano ya Euro 2024, ikiwa ni idadi kubwa zaidi ya mashuti yaliyopigwa na mchezaji yeyote bila bao kwenye michuano mikubwa (ya Kombe la Dunia ama Euro) tangu Kombe la Dunia mwaka 2010 wakati Lionel Messi alipopiga mashuti 29 langoni bila kuifungia bao Argentina.



# KLABU 4 ZA ENGLAND ZINAZOHITAJI SAINI YA COSTA

**LONDON,** England

URENO wana mlinda mlango Diogo Costa wa kushukuru kwa nafasi yao katika robo fainali ya Euro 2024.

Bila ushujaa wake wa hatua ya 16-bora dhidi ya Slovenia, katika muda wa ziada na kuokoa mikwaju ya penalti, mabingwa hao wa 2016 wangewahi zaidi kupanda ndege ya kurudi nyumbani kutoka Ujerumani. (Ingawa tayari wametolewa na Ufaransa kwenye robo fainali).

**Costa, ambaye kwa mara ya kwanza alijiunga na klabu ya sasa ya Porto akiwa mtoto, amekuwa namba moja bila kupingwa tangu 2021, alikuwa kimya hadi mshambuliaji wa Slovenia Benjamin Sesko alipofunga goli akitafuta kushinda katika kipindi cha pili cha muda wa ziada.**

Dakika chache baadaye, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, alikua kipa wa kwanza katika historia ya ubingwa wa Ulaya kuokoa penalti tatu. Ureno ilishinda 3-0 shukrani kwa Crisriano Ronaldo, Bruno Fernandes na Bernardo Silva.

Ni maonesho kama haya kwenye mashindano ya kimataifa ambayo huvutia wachezaji.

Hapo awali Costa alikuwa akivutiwa na Manchester United mnamo 2023 walipokuwa wakitathmini uwezekano wa kuchukua nafasi ya David de Gea kabla ya kumfuata Andre Onana.

Ana kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa pauni milioni 65 katika mkataba uliotiwa saini Novemba 2022, ambayo itakuwa sehemu bora ya kuuza kwa Porto. Kulikuwa na uwezekano wa kukubali ada ya chini msimu uliopita wa majira ya joto huku kukiwa na wasiwasi wa kifedha, lakini maonesho ya Costa kwenye Euro 2024 yanaweza kuongeza ofa, haswa ikiwa kuna ushindani.

Kwa aina ya fedha inayohusika, Ligi Kuu England inaonekana kama ndiko kunakomfaa.

### 4. Wolves

Jose Sa alisaini mkataba mpya wa muda mrefu katika Klabu ya Wolves Septemba mwaka jana, lakini ndani ya miezi michache alikuwa akihusishwa na uhamisho wa pauni milioni 40 kwenda Saudia, ambako kumethibitisha kuwa timu maarufu hivi karibuni kwa wachezaji wa Ureno.

Iwapo Wolves watamuuza Sa kwa fedha nzuri, wanaweza kuwekeza tena kwa mbadala mdogo kama Costa. Wachezaji wote wawili wanawakilishwa na wakala Jorge Mendes na litakuwa jambo la kushangaza tu ikiwa umemsahau Rui Patricio, mtangulizi wa Costa kama namba moja wa Ureno, alitua Wolves mnamo 2018.

Klabu hiyo imeyumba kwa misimu michache kwa hivyo ilikuwa na nia kubwa, lakini ikifikiria kuajiri inaweza kuwa kile wanachohitaji ili kurejea tena Ulaya.

### 3. Newcastle United

Golikipa namba moja wa Newcastle United, Nick Pope alikosa nusu ya msimu uliopita kutokana na jeraha la bega. Bega lile lile aliloteguka hapo awali 2018 alipokosa kampeni nzima kutokana na matokeo hayo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 alikuwa muhimu kwa Magpies kumaliza nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu England msimu wa 2022/23, lakini ikiwa klabu inataka kushindana na mataji unaweza kuwa wakati wa kuimarika.

Tangu PIF ilipoitwaa Newcastle mwaka 2021, wameonesha nia katika soko la uhamisho bila kujiingiza katika matumizi mabaya ya fedha. Uajiri umepimwa na kwa sehemu kubwa, umefanikiwa.

Nguvu ya ulinzi ni nguzo ya kujenga na Costa anaweza kuwa kile Newcastle wanachotafuta.

### 2. Manchester City

Mafanikio ya hivi karibuni ya Manchester City yamechangiwa na kujiamini katika uwezo wao wa kuchukua nafasi ya mchezaji yeyote, huku klabu hiyo ikiwa tayari kumzuia yeyote anayetaka kuondoka. Hatimaye, wachezaji wanapita tu na ujenzi wa kikosi ni kuhusu mabadiliko ya mara kwa mara.

Ederson amekuwa namba moja bila kupingwa wakati wote wa utawala wa Pep Guardiola kwenye Uwanja wa Eithad. Lakini kumekuwa na uvumi katika wiki za hivi karibuni kuhusu mustakabali wake kutokana na kuibuka kwa nia kutoka Saudi Arabia - haswa Al Ittihad. Mbrazil huyo analazimika kuomba uhamisho rasmi, lakini ikiwa kichwa chake kitageuzwa basi huenda City hawatasita kuchukua nafasi yake.

Ederson alikuwa mmoja na wa kwanza kati ya wimbi jipya, jambo ambalo linamfanya Costa wa kiufundi kuwa mteule mzuri wa kujaza glovu na buti zake.

### 1. Chelsea

Licha ya kutumia karibu pauni milioni 40 msimu uliopita kuwanunua Robert Sanchez na Djordje Petrovic, bado kama Chelsea wanahitaji golikipa. Ukizingatia magwiji kama Petr Cech na Thibaut Courtois waliocheza kwenye Uwanja wa Stamford Bridge siku za hivi karibuni walionesha uhodari wao.

Sanchez alijeruhiwa Desemba na, zaidi ya kurejea benchi kwa muda mfupi Machi, alikosa msimu uliobaki. Petrovic basi alichukua nafasi, lakini karatasi safi ilikuwa ngumu kupatikana.

Costa alipewa ofa kwa Chelsea msimu uliopita wa majira ya joto walipokuwa wakitafuta mbadala wa Kepa Arrizabalaga baada ya kukubali kumuuza Edouard Mendy. Lakini walikwenda kwa njia tofauti na mtazamo wa nyuma unaonesha kuwa lilikuwa kosa ambalo wanaweza kulirekebisha kwa kumleta Costa.




COSTA

## Nukuu

"Nadhani kwangu, ni kitu ninachokikubali, juu ya kuwaondoa pepo wa Euro 2020. Unaweza kushindwa mara moja lakini una chaguo ikiwa utajiweka tena katika nafasi hiyo na mimi ni mtu ambaye nitaenda kujiweke mwenyewe katika nafasi hiyo. Nilijiamini na mpira ulipogonga nyavuni nilikuwa mtu mwenye furaha sana," **Bukayo Saka, akielezea furaha yake baada ya kufunga mkwaju wa penalti wakati wakiitoa Uswisi kwa penalti 5-3 hatua ya robo fainali, huku akikumbukia pepo wa Euro 2020, ambapo alikumbana na ubaguzi mkubwa wa rangi kutoka kwa mashabiki wa England baada ya kukosa penalti dhidi ya Italia.**



"Hili ni muhimu kwangu. Naomba msamaha na pona haraka, Pedri! Ni wazi, sikukusudia kukuumiza. Upone haraka na kila la heri. Wewe ni mchezaji mkubwa," **Kiungo wa Ujerumani, Toni Kroos, akiomba msamaha kwa Pedri baada ya kumchezea rafu mbaya, wakati wakitupwa nje na Hispania kwenye mechi ya robo fainali ya Euro 2024 wiki iliyopita. Vipimo vinameonesha amepata majera makubwa.**



"Ufaransa haikustahili kuvuka na wamekuwa wa wastani katika mashindano haya. Lakini ni kutafuta njia katika soka la mashindano," **mshambuliaji wa zamani wa Chelsea na kocha mstaafu, Chris Sutton, ambaye kwa sasa ni mchambuzi wa soka.**



Nipashe Spotika

# MAKOCHA WA5 WAPYA LIGI KUU MSIMU UJAO



FADLU

**Na Adam Fungamwango**

BAADHI ya klabu zimeanza maandalizi ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, huku zingine zikianza leo na zipo zinazosafiri mbali na mikoa yao na nje ya nchi kwa ajili ya 'pre season.'

**Katika maandalizi hayo, baadhi ya timu zina makocha wale wale waliomaliza nao msimu uliopita, lakini zipo zitakazokuwa na wapya kabisa.**

Makocha hao pia wamegawanyika, kwani wapo waliotoka kufundisha klabu za hapa hapa Ligi Kuu, lakini wamechukuliwa kwa ajili ya kuzifundisha zingine, hivyo kwao ni mpya, vile vile kuna watakaofundisha timu ikiwa ni mara ya kwanza kufanya hivyo nchini, wapo pia waliorejea baada ya kufanya hivyo siku za nyuma.

Katika makala haya tunakuletea makocha hao wapya kwenye vikosi, na majukumu wanayotakiwa wanayotakiwa kuyatimiza baada ya kupewa kazi na klabu zao.

### 5# Mecky Maxime - Dodoma Jiji FC

Wiki mbili zilizopita, Dodoma Jiji ilimtangaza Mecky Maxime kuwa kocha wao mkuu, akichukua nafasi ya Francis Baraza ambaye alionyeshwa mlango wa kutokea baada tu ya Ligi Kuu msimu uliopita kumalizika. Kocha huyo mzawa, alikuwa anaifundisha Ihefu, ambayo kwa sasa imebadili jina na kujiita, Singida Black Stars.

Atakuwa na kazi ya kuhakikisha angalau timu hiyo inashiriki Ligi Kuu bila kuwa na presha ya kusaka matokeo ya kubaki Ligi Kuu karibuni kila msimu.

Badala yake iwe timu ambayo hata kama haitamaliza nafasi nne za juu, basi angalau isusubiri mechi za mwisho ndiyo iamue kubaki.

### 4# Mbwana Makata - Prisons

Huyu ndiye atakiongoza kikosi cha Prisons katika Ligi Kuu msimu unaotarajiwa kuanza katikati ya mwezi ujao.

Alitangazwa na klabu hiyo hivi karibuni, akichukua nafasi ya Ahmad Ally ambaye taarifa zinaeleza huenda akawa Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, baada ya kumfurusha, Malale Hamsini mara tu ligi ilipomalizika.

Mbwana Makata naye aliachwa mara tu baada ya kuipandisha Pamba Ligi Kuu kutoka Ligi ya Championship. Kibarua chake kikubwa kocha huyo mzawa ni kuhakikisha Prisons haihangaiki kupigania uhai wa kubaki kwenye ligi na timu zikizo chini ya msimamo, badala yake ipiganie angalau moja kati ya nafasi nne za juu kama ilivyokuwa enzi zake.

### 3# Goran Kopunovic - Pamba

Mserbia huyu atakuwa na kibarua cha kuhakikisha walau Pamba inasalia Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, ili ijipange tena kwa msimu wa pili.

Pamba ambayo itacheza Ligi Kuu msimu huu baada ya miaka 23, viongozi wake hawatokubali kuona inasuasua kwani wanajua ikishuka daraja inaweza kuwachukua tena muda mrefu kurejea.

Ndiyo maana ilipopanda, ilimuondoa Makata na kumleta kocha mzoefu, Goran Kopunovic, kuchukua nafasi hiyo.

Ni kocha ambaye alishawahi kuifundisha Simba mwaka 2015, alirejeshwa nchini na kuinoa Klabu ya Tabora United, ambapo hakufanya vema kutokana na sababu mbalimbali, akaondoka kabla ya kuibukia timu hiyo.

### 2# Patrick Aussems - Singida Black Stars

Pamoja na kwamba atakuwa kocha mpya wa Singida Black Stars, lakini si mgeni kwenye Ligi Kuu.

Anarejea nchini baada ya miaka mitano kupita, awali akiifundisha Simba, kuanzia 2018 hadi 2019, kabla ya kutimkia Black Leopards ya Afrika Kusini na baadaye AFC Leopards ya Kenya.

Patrick Aussems raia wa Ubelgiji amerejeshwa tena nchini kuchukua mikoba ya Maxime, ambaye kwa sasa yupo Dodoma Jiji.

Kutokana na usajili ambao klabu hiyo imeufanya na aina ya wachezaji ilionao, viongozi wake hawatomuelewa kocha huyo kama timu hiyo haitomaliza kwenye nafasi nne za juu msimu ujao.

### 1# Fadlu Davids - Simba

Jina lake kamili Fadluraghman Davids, raia wa Afrika Kusini, kocha pekee kati ya wote hawa ambaye hajafundisha timu yoyote nchini.

Ndiye kwa sasa Kocha Mkuu wa Simba, anayechukua nafasi ya Abdelhak Benchikha raia wa Algeria ambaye aliondoka kabla ya ligi kumalizika na timu kukaimiwa na mzawa, Juma Mgunda.

Ni kocha mzoefu kwenye soka la Afrika, akiwa amezifundisha klabu mbalimbali kubwa kama Maritzburg United na Orlando Pirates zote za Afrika Kusini, akiwa kama kocha msaidizi na baadaye mkuu, baada ya waliokuwa juu yake Milutin Sredojevic 'Micho', Rulani Mokwena, na Josef Zinnbauer kuchukuliwa na klabu zingine.

Amewahi pia kuwa kocha msaidizi wa Lokomotiv Moscow ya Urusi, na anajiunga na Simba akitoka kuwa kocha msaidizi wa Raja Casablaca ya Morocco, chini ya Mjerumani, Zinnbauer, aliyeamua kumchukua tena baada ya kuachana naye, Orlando Pitares.

Ana kibarua kizito cha kuionganisha Simba ambayo inaonekana kuwa na idadi kubwa ya wachezaji wapya inayowasajili, huku viongozi, wanachama na mashabiki wakiwa na matumaini makubwa ya kufanya vema msimu ujao, baada ya misimu mitatu ya huzuni.

Anatakiwa kufanya mambo yafuatayo, kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu, kama ikishidikana nafasi ya pili, kutwa mataji nje ya ubingwa wa Bara, pamoja na angalau kutinga nusu fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

**JE, WAJUA?**



USHINDI wa England dhidi ya Uswisi kwenye robo fainali ya michuano ya Euro 2024 juzi, Jumamosi umeifanya kuwa taifa la sita Ulaya kushinda mechi 50 katika mashindano makubwa ya kimataifa baada ya Ujerumani, Italia, Ufaransa, Hispania, na Uholanzi.

HABARI KITAIFA

# EPZA yajikita kukuza ushindani kibiashara

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), imesema inaendelea kuweka juhudi kubwa katika uzalishaji wa bidhaa shindani za viwandani ili kusaidia nchi kukuza ushindani wa kibiashara katika soko la kimataifa.

Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Charles Itembe, alisema hayo katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara (DITF) maarufu Sababasa yanayoendelea jijini Dar es Salaam.

"Uzalishaji wa bidhaa zilizoongezwa thamani ni muhimu sana katika kujenga uwezo wa nchi kushindana katika soko la dunia na pia kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni," alisema.

Alisema serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia wawekezaji wengi zaidi hasa kwenye sekta ya viwanda.

Juhudi hizi zimeonekana kutokana na ongezeko kubwa la wawekezaji nchini hali ambayo imelazimu EPZA kuendelea kujenga maeneo mengi zaidi ya viwanda hasa kupitia programu zake za EPZ na SEZ.

Katika maeneo hayo, EPZA imekuwa ikifanya juhudi kuweka miundombinu ya msingi kama maji, barabara na umeme ili iwe rahisi kwa wawekezaji kuingia kwa urahisi zaidi.

"Ikumbukwe kwamba biashara za mipakani zimerahisishwa kwa kiasi kikubwa hivyo kama nchi haitaamka na kuimarisha sekta ya uzalishaji bidhaa nje ya nchi haitanufaika na mikataba ya kiuchumi ambayo serikali imeendelea kuingia," alisema.

Alisema Tanzania si kisiwa, hivyo nchi haiwezi kujitenga na kufanya mambo yake yenyewe, kutokana na hali hiyo, nchi lazima iwe na mipango madhubuti ya kuepuka kuwa soko la bidhaa za nchi zingine bali iweze kuzalisha na kuuza katika nchi hizo na moja ya taasisi yenye jukumu la kuweka mazingira hayo wezeshi ni EPZA.

Taasisi hii imeundwa ili kufikia malengo haya ya serikali ya kuongeza uzalishaji wa bidhaa zilizoongezwa thamani kupitia programu za EPZ na SEZ.

Alisema programu za EPZ na SEZ zimekuwa na mafanikio makubwa katika nchi ya Asia kwa kuvutia uwekezaji mkubwa katika sekta viwanda, kuongeza thamani ya bidhaa kwa mauzo nje na kuziongezea pato lao la fedha za kigeni.

Jukumu la EPZA ni kusaidia uzalishaji wa bidhaa zinazouzwa nje ya nchi, kwa sababu ndio mlango pekee wenye afya unaoweza kuliingizia taifa mabilioni ya fedha za kigeni katika uchumi.

Mkurugenzi huyo wa EPZA alisema, kasi ya uwekezaji kupitia Mamlaka ya EPZ inazidi kuongezeka, jambo muhimu linaloendelea hivi sasa ni kuandaa maeneo Maalum ya Viwanda na kuyapatia miundombinu muhimu ya barabara, umeme na maji na maandalizi ya maeneo ya uwekezaji ni ya EPZA.

Malengo makubwa yakiwa ni kuhakikisha malighafi zote za nchi zinachakatwa kabla ya kuuzwa nje ya nchi, kwa sababu katika ulimwengu wa kisasa ni aibu kwa nchi kama Tanzania kuuza bidhaa zikiwa ghafi nje ya nchi, miongoni mwa mipango iliyojiwekea EPZA ni kusajili kampuni nyingi za nje ili kufikia malengo.




Mkuu wa Idara ya Broadband Halotel Tanzania, Freddy Ndabila akiwa katika banda la Halotel sabasaba akielezea kuhusu huduma mpya ya Halofiber kutoka Halotel ili kuboresha huduma za Internet Halofiber **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

# Gairo kuanza uzalishaji parachichi, tumbaku

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Gairo, mkoani Morogoro, Jabir Makame amesema, wilaya hiyo imeweka mikakati ya kuanza kilimo cha uzalishaji wa mazao ya kimkakati yakiwamo parachichi na tumbaku ili wananchi waweze kuondokana na umasikini na kuongeza vyanzo vipya vya mapato.

Zao la parachichi linastawi katika ukanda wa Tarafa ya Nongwe na wilaya hiyo imejipanga hadi kufikia mwishoni mwa mwaka huu (2024) kuwa na idadi ya miche isiyopungua 240,000 iliyopandwa sawa na ekari zaidi ya 2,000 ya zao hilo.

Makame alisema hayo mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima wakati wa kikao cha baraza maalum la madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo ambacho ni cha kikatiba kupitia na kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema wilaya imewekeza zao la parachichi katika ukanda wa Tarafa ya Nongwe pamoja na zao la tumbaku kwenye ukanda wa Tarafa ya Gairo.

Mkuu wa wilaya alisema kwa zao la parachichi miche zaidi ya 40,000 imepandwa kupitia mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na miradi ya wananchi wenyewe pamoja na nguvu ya Mbunge wa Jimbo la Gairo.

Aidha, wilaya inashirikiana na Taasisi ya Agriwezesha na inatarajia hadi kufikia mwezi Desemba, mwaka huu idadi ya miche 160,000 itatolewa bure kwa wananchi katika mashamba yao.

Mkuu wa Wilaya alisema kupitia halmashauri hiyo, katika bajeti yake ya ndani wanatarajia kuzalisha miche zaidi ya 80,000.

Alisema kutokana na mkakati huo katika kipindi cha miaka mitatu au minne ijayo halmashauri hiyo itakuwa inajikusanyia mapato ya kutosha kupitia uwekezaji wa kilimo cha zao hilo.

Kuhusu tumbaku alisema ili kuhakikisha dhamira ya kilimo hicho inatimia, kikao cha kimkakati kilishafanyika na kimeweka dira na mwelekeo mpya wa kilimo hicho katika wilaya hiyo.

Alisema kikao hicho kiliwakutanisha wadau wote wa mnyororo wa thamani wa zao hilo wakiwamo Taasisi ya Utafiti wa Tumbaku Tanzania (TORITA), Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB) na Kampuni ya Usindikaji wa Tumbaku (Mkwawa Leaf).

# VETA kuwafunza 'mahausi geli' kuhudumia wazee, watoto

**Na Christina Mwakangale**

MAMLAKA ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), imekuja na mtaala maalumu kwa ajili ya kuwafunza wanaofanya kazi za ndani 'mahausigeli' ili kumudu kuwahudumia watoto na wazee pamoja na kuwaandaa kufanya kazi nje ya nchi.

Kadhalika, imesema inatarajiwa kuongeza idadi ya vituo vya mafunzo kutoka vilivyokuwapo awali 29 mwaka 2020 na vitafikia 143 mwaka 2025, kutokana na kukua kwa mahitaji katika wilaya na mikoa yote nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Anthony Kasore, aliyasema hayo alipotembelea Banda la VETA jana na kuzungumza na waandishi wa habari kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), maarufu Sabasaba.

"VETA tumeleta vitu mbalimbali kuendana na nia ya maonesho, kama vile huduma tunazotoa katika vyuo vyetu, kama eneo hitaji la mafunzo kwa wanaofanya kazi za ndani, mtaala utawasaidia Watanzania kupata mafunzo kuhudumia watoto, wazee.

"Mtu anafundishwa hadi kupika na tumeona kuna ambao wanahitaji kwenda nje ya nchi kufanya kazi kama hii, ili watambulike kuwa na vyeti tukaona vyema kuwa na hili na wao wawe na ajira inayotambulika," alibainisha Kasore.

Pia, alisema upo mtaala unaotoa mafunzo ya namna ya kutengeneza vifaa tiba, kwa kuanzia Mkoa wa Mara na Geita huku wakijikita kwa kuwa na mtaala wa watu wanaofanya kazi viwandani kwa kutumia mitambo ya kompyuta.

"Kozi hii imeanza Desemba, mwaka jana, hasa kwa ambao wamemaliza vyuo kwa ngazi mbalimbali. Wawekezaji wanakuja nchini sasa hawatapata shida kupata watu wa kusimika mitambo na kuifanyia marekebisho, pia hatujaacha kuwaatamia wabunifu," aliongeza.

Kasore alisema vipo vifaa saidizi kama vya kumenya viazi kwa dakika moja vya kilo moja, hususan kwa ambao wanakaanga viazi kwa magunia mengi kwenye biashara zao kila siku, badala ya kupoteza muda kwa kutumia visu.

"Wenye mahitaji maalumu msiwafungie ndani, mlete mtoto, mzee, kijana tumpe mafunzo. Lazima tuwe na taifa lenye ubunifu, balbu ikiungua nyumbani uweze kubadilisha mwenyewe sio hadi uite fundi."

Pia, alisema wazazi na walezi pamoja na wazee waliostaafu, wafike VETA kujifunza ujuzi aina yoyote, ili kuwafanya wawe na shughuli ya kuushughulisha mwili pia na kujiongeza kipato.






JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika mahakama ya mwanzo Wilaya ya GEITA

Kituo cha NYANKUMBU Mkoa GEITA

Shauri la Madai Na. 99/2024

Jina la mdai NKWABI MBOJE

Jina la mdaiwa LAMECK GIBSON KATORWA

KUITWA SHAURINI MDAIWA
(kanuni ya 18 za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)

**Kwa : LAMECK GIBSON KATORWA WA GEITA**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta /wameleta madai yake/yao kwamba ( Eleza hapa habari za Madai)
**MADAI YA FEDHA TSHS 1,715,000/=**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 16 mwezi 07 mwaka 2024 saa2:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 03 mwezi 07 mwaka 2024

RESIDENT MAGISTRATE


# India kuwekeza uchakataji taka, kuzalisha mbolea

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imeanza mazungumzo na wawekezaji kutoka nchini India ili kuanza kulitumia dampo la jiji hilo kuchakata taka zinazooza na kuzalisha mbolea.

Mazungumzo hayo yalianza kufanyika juzi ambapo menejimenti ya halmashauri hiyo na wawakilishi wa kampuni ya BA Prerna Clean Earth walikutaka kwa ajili ya kujadiliana namna ya kutekeleza mradi huo.

Mwakilishi wa kampuni hiyo, Parish Karathia alisema endapo watakubaliana wanakusudia kuzalisha mbolea ambayo itatumika mashambani na hivyo kulifanya dampo hilo kuwa na faida zaidi ya ilivyo sasa.

"Tutatenganisha taka ngumu na hizi ambazo zinaoza, tutazalisha mbolea ambayo wakulima wataitumia shambani, hapa faida ya hizi taka itaonekana," alisema Karathia.

Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, John Nchimbi alisema baada ya kupokea ombi la kampuni hiyo walijadiliana na kukubaliana kulipeleka ngazi za juu kwa ajili ya kuchakatwa zaidi kabla ya kuanza kuingia makubaliano rasmi.

Alisema endapo jambo hilo litaridhiwa wao watasaini mkataba wa namna ya kushirikiana kutekeleza mradi huo, huku akisisitiza kwamba uwekezaji kama huo umefanyika katia mikoa ya Kilimanjaro na Dar es salaam na manufaa yanaonekana.

Alisema mradi huo utakuwa miongoni mwa vyanzo vya uhakika vya mapato ya halmashauri hiyo pamoja na kuwanufaisha wakulima kwa kupata mbolea ya uhakika.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.
(Together we can build a better life)

PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

PURSUANT TO REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014 AND REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER

| S/N | DESCRIPTION | | FEES AND CHARGES TZS | USD |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Monthly Maintanance | SA | 2,000.00 | 2 |
| | | CA | 6,000.00 | 4 |
| 2 | Non Maintanance of Minimum Balance | SA | 1,500.00 | 2 |
| | | CA | 4,000.00 | 4 |
| 3 | Account Statement Charges | SA-Monthly | - | 0 |
| | | SA-Interim | 1,500.00 per page | 1.5 per page |
| | | CA-Monthly | Free | Free |
| | | CA-Interim | 1,500.00 per page | 1.5 per page |
| 4 | Cash withdrawal | SA-Up 25M | Free | |
| | | SA-Over 25M | 0.26% | |
| | | SA-Up to $2K | | Free |
| | | SA-$2K-$5K | | 0.60% |
| | | SA-Over $5k | | 0.60% |
| | | CA-Up to 25 M | Free | |
| | | CA-Above 25M | 0.26% | |
| | | CA-Up to USD 5K | | Free |
| | | CA-$ 5K-$10K | | 0.60% |
| | | CA-Above $ 10K | | 0.60% |
| 5 | Cash Deposit Charges | SA-Up to 25M | Free | |
| | | SA-Over 25M | 0.22% | |
| | | SA-Up $5K | | Free |
| | | SA-Over $5K | | 0.50% |
| | | SA-small currency ($1 to $20) | | 10.00% Minimum charge $1 |
| | | CA-Up to 50M | Free | |
| | | CA-Over 50M | 0.22% | |
| | | CA-Up to $10K | | Free |
| | | CA-Over $10K | | 0.50% |
| | | CA-small currency ($1 to $20) | | 10.00% Minimum charge $1 |
| 6 | Balance Confirmation Certificate | SA | 12,800.00 | 10 |
| | | CA | 21,200.00 | 13 |
| 7 | Account Closure Charges | SA | 20,000.00 | 20 |
| | | CA | 50,000.00 | 50 |
| 8 | Activation of Dormant Account | SA | Free | Free |
| | | CA | Free | Free |
| 9 | Stop Payment Charges | SA | Free | Free |
| | | CA | 35,000.00 | 28 |
| 10 | Cheque Return Charges/Dishonoured Cheque | CA-Inward | 50,000.00 | 50 |
| | | CA-Outward | 50,000.00 | 50 |
| 11 | Cheque Clearing Charges | CA-Inward | 1,300.00 | 1 |
| | | CA-Outward | Free | Free |
| 12 | Ledger folio charges per folio (40lines per | SA | Free | Free |
| | | CA | 6,000.00 | 4.00 |
| 13 | Cheque book Charges | CA-50 Leaves | 42,000.00 | 27 |
| 14 | Mobile Banking | | | |
| i | Withdrawal Charge | Upto 100,000 | 1,700.00 | N/A |
| | | 101,000 to 200,000 | 2,600.00 | N/A |
| | | 201,000 to 400,000 | 4,300.00 | N/A |
| | | 401,000 to 600,000 | 5,100.00 | N/A |
| | | 601,000 to 999,000 | 6,800.00 | N/A |
| ii | Funds Transfer/Mobile Wallet | Upto 100,000 | 500.00 | N/A |
| | | 101,000 to 250,000 | 900.00 | N/A |
| | | 251,000 to 500,000 | 1,700.00 | N/A |
| | | 501,000 to 1,000,000 | 4,300.00 | N/A |
| | | 1,001,000 TO 10 Mn | 8,500.00 | N/A |
| 15 | Locker Rent-Yearly | Small | 296,700.00 | N/A |
| | | Medium | 508,500.00 | N/A |
| | | Big | 635,600.00 | N/A |
| 16 | Remittances | | | |
| i | TISS | Any amount per 1 | TZS 8,450.00 | TZS 8,450.00 Equivallent |
| ii | E Remittances | Upto USD 1000 or Eq. TZS | 17,000.00 | $ 9.00 |
| | | 1001 to 5000 | 20,400.00 | $ 11.00 |
| | | 5001 to 10000 | 40,700.00 | $ 22.00 |
| | | 10,001 and above | 84,800.00 | $ 43.00 |
| iii | Swift Outward | Upto 5,000 | NA | $ 39.00 |
| | | 5,001 to 10,000 | NA | $ 51.00 |
| | | above 10,000 | NA | $ 77.00 |
| iv | Swift Inward | Upto 5,000 | NA | $ 11.00 |
| | | 5,001 to 10,000 | NA | $ 16.00 |
| | | above 10,000 | NA | $ 26.00 |

| S/N | DESCRIPTION | | FEES AND CHARGES TZS | USD |
|---|---|---|---|---|
| 17 | Loan/Advances Related Charges | | | |
| i | Processing Charges | Upto 5 Mio - | 21,200.00 | |
| | | 5Mio to 10 Mio - | 169,500.00 | |
| | | 10 Mio to 25mio - | 339,000.00 | |
| | | 25 mn to 500 mio - | 1.28% | |
| | | >500mio--* (*minimum 7.5mio) | 1.06% | |
| | | Upto 5,000 - | | $85.00 |
| | | 5000 to 10,000 - | | $170.00 |
| | | Upto 20,000 - | | $255.00 |
| | | 20,000 to 500,000 - | | 1.28% |
| | | >500,000--* | | 1.06% |
| ii | Documentation Charges | Upto 100 MILLION | FREE | |
| | | >100 Mio (-Min 300,000) | 0.26% | |
| | | Upto 50,000 | | FREE |
| | | >50,000 - (Min 150) | | 0.26% |
| iii | Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - | 21,200.00 | |
| | | 5 Mio to 10 Mio - | 169,500.00 | |
| | | 10Mio 25mio - | 381,400.00 | |
| | | 25 mn to 500 mio - | 1.53% | |
| | | >500mio--* (*minimum 9mio) | 1.28% | |
| | | Upto 20,000 - | | $255.00 |
| | | 20,000 to 500,000 - | | 1.53% |
| | | >500,000--* (*minimum 9000) | | 1.28% |
| iv | Inspection Charges | Upto 100 Mio - | 21,200.00 | |
| | | >100 mio - | 42,400.00 | |
| | | Upto 50,000 | | $22.00 |
| | | >50,000 | | $43.00 |
| v | Credit Reference Report Charges | | 101,700.00 | $43.00 |
| vi | Pre-payment penalty | Calculated as %ge pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders | 2.00% | 2.00% |
| 18 | Guarantees (Local & International) | | | |
| i | Bonds & Guarantees | per quarter (Min TZS 75,000) | 1.02% | 1.02% |
| ii | Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | per quarter (Min TZS 75,000) | 0.43% | 0.43% |
| 19 | Letter of Credit | | | |
| 19.1 | Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof) | | | |
| i | Opening commission | commission Min $ 200 | NA | |
| ii | LC amendment Commission | Commision Min $50 max 350 | NA | 1.02% |
| iii | Swift charge for LC opening | | NA | 0.34% |
| iv | Swift charge for other message/amendments | | NA | $34.00 |
| v | Extensions - Commissions | commission Min $ 200 | NA | $34.00 |
| vi | LC cancellation charges | commission Min $ 200 | NA | 1.02% |
| vii | Non payment of Bills on due date | Till Payment | NA | 1.02% |
| 19.2 | Export Letters of Credit (per quarter or part thereof) | | | |
| i | Advising commission | | NA | $119.00 |
| ii | Confirmation Commission | Commision Min $150 | NA | 0.43% |
| iii | Negotiating bills under LC | Commision Min $75+cuourier+interest | NA | 0.43% |
| iv | Reimbursement claim paid | Commision Min $75 | NA | 0.43% |
| v | Extensions - | Commision Min $200 | NA | 1.02% |
| vi | Collection of Export LC | Commision Min $75+cuourier+interest | NA | 0.43% |
| vii | Amendments | | NA | $64.00 |
| 20 | Other disclosures | | | |
| i | Base or Prime Lending Rate | | 16% | 10% |
| ii | Maximum spread | | 5% | 5% |
| iii | Penal Interest | | | |
| | a.For non compliance on Terms of Saction | Rate per year over regular rate of interest | 3% | 3% |
| | b.For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | Rate per year over regular rate of interest | 5% | 5% |
| vi | Deposit Rates | | | |
| | a. Current account | | Nill | Nill |
| | b. Savings bank deposit | | 3.00% | 1.00% |
| | C. Fixed Deposits Rates | Up to TZS 50 M(up to USD 50,000) | | |
| | | 30 -90days | 3.50% | 1.50% |
| | | 91-180days | 4.50% | 2.25% |
| | | 181-364 days | 5.50% | 3.00% |
| | | 1 year and above | 8.00% | 3.75% |
| | | 2 Years and Above | 8.00% | 4.00% |
| | | TZS 50 M-100M (USD 50,000 -USD 100,000) | | |
| | | 30 -90days | 4.50% | 2.25% |
| | | 91-180days | 5.50% | 2.50% |
| | | 181-364 days | 7.00% | 3.50% |
| | | 1 year and above | 8.25% | 4.25% |
| | | 2 Years and Above | 9.00% | 4.75% |
| | | Above 100 M(Above USD 100,000) | | |
| | | 30 -90days | 5.50% | 2.50% |
| | | 91-180days | 6.50% | 3.25% |
| | | 181-364 days | 7.50% | 4.00% |
| | | 1 year and above | 8.50% | 4.75% |
| | | 2 Years and Above | 9.50% | 5.00% |

| | |
|---|---|
| HEAD TREASURY AND TRADE FINANCE | 04-Jul -24 |
| GM-CREDIT | 04-Jul -24 |
| HEAD BUSINESS OPERATIONS | 04-Jul -24 |


# Wafanyakazi waliogoma kisa mshahara warejea kazini

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAFANYAKAZI wa Kiwanda cha Chai Kibena kilichopo katika Halmashauri ya Mji wa Njombe, waliokuwa wamegoma kufanya kazi kwa zaidi ya siku tano, wamerejea kazini baada ya mwajiri wao kulipa mishahara waliyokuwa wanadai zaidi ya Sh. milioni 200.

Wafanyakazi hao walirejea kazini mwishoni mwa wiki kwenye kikao baina yao na viongozi wa kampuni hiyo kilichoitishwa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka na kufanyika kiwandani hapo kwa lengo la kutafuta suluhu.

Mkurugenzi wa kampuni ya DL Group Tanzania, Jamerson Moturi alikiri wafanya kazi hao kutolipwa mishahara yao kwa kipindi cha miezi minne.

"Leo Julai tano tunalipa mshahara mmoja ambao ni Sh. milioni 200.1 na wiki ijayo Julai 11 tunalipa mshahara mwingine wa miezi miwili Sh. milioni 400 na Agosti nane tutalipa mshahara mwingine na kukamilisha," alisema Moturi.

Alisema walishindwa kuwalipa wafanyakazi hao mishahara kutokana na zao hilo kukabiliwa tatizo la bei duniani hali inayosababisha gharama ya kusafirisha kuwa kubwa na hivyo kukigharimu kiwanda bei kubwa. Mkuu wa Mkoa wa Njombe,

Anthony Mtaka alisema jambo la kutokulipwa mshahara wafanyakazi hao linafedhehesha kwa sababu mshahara ni kipato kinachosaidia wao kutekeleza majukumu yao.

"Mnaendesha maisha, mnapeleka watoto shule, mnajitibia lakini mambo mengine yanaenda bila ya kuwa ombaomba," alisema Mtaka.

Mtaka alimshauri mwekezaji huyo kuwa na chanzo mbadala cha mapato ili kuwa na uwezo wa kulipa wafanyakazi mishahara kwa wakati bila ya kusababisha migogoro.

Awali, mwakilishi wa Bodi ya Chai Tanzania, Theophord Ndunguru alisema walipata taarifa ya wafanyakazi wa viwanda hivyo kutolipwa ambavyo ni Ikanga Lupembe, Luponde na Kibena kutokulipwa mishahara yao.

Ndunguru alisema kwamba tasnia ya chai duniani hali ni mbaya kwa sababu bei zimeshuka tofauti na ilivyokuwa awali.

"Wenzetu Kenya kuna viwanda tisa vimefungwa kwa sababu ya hali hiyo, Uganda kuna viwanda saba wamefunga na hapa kwetu kuna baadhi wamefunga pia kwa sababu walikuwa wanaona wanapata hasara," alisema Ndunguru.

Aliongeza kuwa: "Sasa DL naye alikuwa kwenye harakati hizo lakini kwa kuangalia maslahi mapana ya nchi, wafanyakazi na wakulima akaona aendelee, huku anasuasua matokeo yake ni kwamba akashindwa kulipa mishahara," alisema Ndunguru.

Alisema kufuatia vikao vya wafanyakazi na viongozi wao katika viwanda hivyo vitatu walikubaliana kurudi kazini pindi tu watakapoingiziwa mishahara yao.



# 'Serikali kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema serikali itaendelea kuchukua hatua za kukuza utalii nchini, ikiwemo kuweka mazingira bora ya uwekezaji na kuvitangaza vivutio vya utalii vya Zanzibar katika ngazi za kimataifa.

Aliyasema hayo jana katika mahafali ya tatu ya Kituo cha Kutolea Mafunzo ya Utalii Michamvi yaliyofanyika Mjini Zanzibar.

Alisema juhudi zinazochukuliwa na serikali katika kuimarisha na kukuza sekta ya utalii zimesaidia kukua kwa uwekezaji kama vile ujenzi wa hoteli na nyumba za kulala wageni ambazo zinachangia kutoa fursa za ajira kwa vijana.

Hemed alisema serikali itaendelea kuimarisha vivutio vya utalii ili kuwasaidia vijana kujiajiri, hivyo aliwataka vijana wa Zanzibar kuzichangamkia fursa zilizopo ili kuendana na soko la dunia .

Pia, aliwataka wahitimu kutumia vyema elimu waliyoipata kutafuta fursa za ajira katika sekta ya utalii na nyinginezo sambamba na kuendelea kujifunza na kujiendeleza katika elimu ya juu kwa kipindi hiki ambacho serikali imeongeza fursa za mikopo ya elimu ya juu kwa ngazi mbalimbali.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa alisema: "Pia nalipongeza Shirika la Umoja wa Mataifa la Kusaidia Watoto (UNICEF) kwa kutoa ushirikiano katika kuhakikisha wanafunzi 250 wanakamilisha masomo kwa kiwango kizuri ambacho kitawasaidia katika kupambana na soko la ajira ndani na nje ya nchi".

Pia, aliutaka uongozi wa chuo cha ZCET, kuwafundisha wanafunzi kwa kuzingatia utamaduni wa kizanzibari katika nyanja ya mavazi, chakula na namna ya kuwahudumia wageni kwa ukarimu ili kuendelea kulinda hadhi na heshima ya Zanzibar.

Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Kutolea Mafunzo ya Utalii Michanvi, Taufiq Salum Turky alisema lengo la kituo hicho ni kuisaidia jamii na kuihuwisha katika kufikia maendeleo, hasa kwa vijana waliokuwa hawapo katika mfumo rasmi wa elimu kuwapatia ujuzi na kuweza kujiajiri.

Turkey alisema kuanzishwa kwa kituo hicho ni matokeo ya kuona kuwa Zanzibar kuna fursa nyingi kupitia sekta ya utalii na asilimia 60 ya wanaofanya kazi katika sekta ya utalii siyo Wazanzibari, hivyo vijana wana fursa kubwa ya kutimiza malengo yao kupitia utalii.

Mwakilishi Mkaazi wa UNICEF, Lacksin Bawani alisema UNICEF kwa kushirikiana na Global Affairs Canada inaendelea kutoa usaidizi wa kiufundi na kifedha ili kuhakikisha kila msichana mdogo anajifunza na kutimiza malengo yake ya maisha.

# EU, EIB yatoa msaada tril.1/- kusaidia wakulima

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMUIYA ya Umoja wa Ulaya (EU) na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) wametoa msaada wa Sh. trilioni 1.044 kwa ajili ya kuziwezesha taasisi za kibenki nchini kutoa mikopo kwa wajasiriamali na vikundi vya uzalishaji katika sekta ya uchumi wa bluu.

Mojawapo ya makundi yatakayonufaika na mkopo huo ni wajasiriamali wa kilimo cha mazao ya baharini visiwani Zanzibar.

Akizungumza visiwani Zanzibar mwishoni mwa wiki katika hafla ya utiaji saini wa makubaliano ya mkataba wa kutolewa kwa fedha hizo, Makamu wa Rais wa EIB, Thomas Ostros, alisema benki hiyo inaunga mkono juhudi zinazochukuliwa na serikali ya Tanzania na Zanzibar katika kukuza uchumi na kuweka kipaumbele uchumi wa bluu kwa uzalishaji wa mazao ya baharini.

Alisema wakulima wa mwani visiwani Zanzibar wanajitahidi kulima ambapo kilimo hicho kimewajumuisha kwa asilimia kubwa wanawake katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo, hatua ambazo ni sehemu ya mikakati ya usawa wa kijinsia katika uzalishaji.

Aidha, alisema wafanyabiashara wadogo ndiyo kiunganishi cha uchumi wa nchi nyingi Afrika ambapo wanao uwezo mkubwa wa kuzalisha ajira kwa kuendesha familia zao. Pia, alisema wataendelea kuunga mkono juhudi za Tanzania katika kuwawezesha wafanyabiashara wadogo ambapo mwaka jana benki hiyo ilitoa Sh. bilioni 775, huku Tanzania ikiongoza katika nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara kunufaika na misaada hiyo.

Alisema juhudi hizo zimesaidia kuwainua wafanyabiashara wadogo kwa kuwaunganisha na taasisi za fedha kupata mikopo nafuu kuendesha shughuli za kibiashara na kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Naibu Balozi wa EU, Emilio Rossette, alisema wataendelea kuiunga mkono Tanzania katika misaada ya aina mbalimbali ikiwemo ya mabadiliko ya tabia ya nchi na athari zake.

"Umoja wa Ulaya tunaridhishwa na juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Tanzania katika sekta mbalimbali za maendeleo ambapo kwa sasa tumejikita katika maeneo ya mabadiliko ya tabia ya nchi" alisema.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Bluu Zanzibar, Zahoro Kassim El-Kharousy, alisema miongoni mwa vipaumbele vya Serikali ya Zanzibar ni uchumi wa bluu kwa ajili ya kuwainua wajasiriamali wadogo kujikomboa kiuchumi na kupiga hatua za kimaendeleo.

Zahoro alisema ni faraja kubwa Tanzania kupata fedha hizo kwa ajili ya uwekezaji wa uchumi wa bluu.

Katika mgawanyo wa fedha hizo unaonesha kwamba Sh. bilioni 458 zimepelekwa Benki ya KCB, Sh.bilioni 430 zitakwenda Benki ya CRDB na Sh.bilioni 287 Benki ya NMB.




Makamu wa Rais wa Benki ya uwekezaji ya Ulaya (EIB) Thomas Ostros (katikati) akionesha hati ya makubaliano yaliyotiwa saini ambapo benki hiyo pamoja na Jumuiya ya Ulaya zimetoa jumla ya Sh.trilioni 1.043 ambazo zitakwenda katika mabenki kwa ajili ya kuwawezesha wafanyabiashara wadogo katika uchumi wa buluu kupata mikopo.Kulia ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu Zahoro Al-Kharousy na kushoto ni Naibu Balozi wa Jumuiya ya Ulaya, Emilio Rossette. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Jafo awahakikishia ushirikiano wafanyabiashara

**Na Joseph Mwendapole,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, ameihakikishia sekta binafsi hususani wafanyabiashara na wawekezaji wa viwanda kuwa atashirikiana nao kutatua changamoto mbalimbali za kibiashara.

Alitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na baadhi ya taasisi zilizo chini anayoiongoza, zinazofanya kazi kwa ushirikano kati ya Tanzania Bara na visiwani, zinazohusika na masuala ya biashara baada ya kuapishwa Ikulu ndogo Tunguu, Zanzibar.

Dk. Jafo alitoa wito kwa wizara na sekta binafsi bara na visiwani kushirikiana kwa karibu na wizara yake ili kukuza sekta ya viwanda na biashara na kufikia malengo ya serikali ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda.

Vilevile, aliahidi kuendelea kushughulikia matatizo yanayowakabili wafanyabiashara, wamiliki wa viwanda na sekta binafsi kwa ujumla ili waweze kuzalisha kwa wingi na kuuza na hatimaye serikali kuendelea kukusanya mapato ya kodi.

Alisema sekta binafsi imeajiri watu wengi zaidi nchini, hivyo iwapo itawekewa mazingira mazuri itaendelea kustawi na kuongeza idadi ya ajira kwa Watanzania, pato la taifa na kujenga uchumi imara na shindani wa viwanda.

Dk. Jaffo alisema yeye na wataalamu wake ataendelea kukutana na wafanyabiashara mbalimbali kupitia mabaraza ya biashara katika mikoa yote nchini, kwa lengo la kusikiliza changamoto zao na kujipanga jinsi ya kuzitatua ili kuhakikisha sekta ya viwanda na biashara inakua kwa kasi.

Aidha, aliagiza kila mtumishi wa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na taasisi zake kutimiza wajibu kwa weledi na ufanisi ili kuhakikisha wizara hiyo inafikia matarajio ya serikali katika kukuza sekta ya viwanda na biashara.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE
Kituo cha JUMUISHI mkoa wa DAR ES SALAAM
Shauri la ndoa na.906/2024
Jina la mdai ALIKIPO M. NDARO
Jina la mdaiwa MAWAZO SEIF KADUGUDA

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za utaratibu wa madai katika mahakama za mwanzo)**

**Kwa: MAWAZO SEIF KADUGUDA**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba........ TALAKA**

Kwahiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 10 mwezi 7 mwaka 2024 saa2 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahuidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea

ANGALIZO:kama hautohudhuria siku ikiyotajwa hapo juu ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa mahakama leo tarehe 1 mwez 7 mwaka 2024

HAKIMU

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 14030 OF 2024
In the matter of the Estate of the late
CASTOR MARTIN SAMATI
Of Ipagala within Dodoma Region
AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ANNA RAPHAEL LUGENDO

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 18 Day of 7, 2024

Presented for filling this 20 Day of JUNE, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI


**APE ENGINEERS SERVICES**

WANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI T770ARE AINA YA FUSO MITSUBISHI ,CHASISI NAMBA FK417H542788 KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU YAKE POLISI TAARIFA

**PHQ/IRI/IRI/239/2024**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**BAKARI SHABANI BAKARI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1626-0046 kilicho tolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya MARIADO mwaka 2019. Yeyote atakaye kiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa **PHQ/DAR/KIN/135102/2024**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO
YA WILAYA YA MOROGORO
KITUO CHA KINGOLWIRA
MKOA WA MOROGORO
Usimamizi wa Mirathi Na...2/2024
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU: NURU JUMA MWEVIRA wa MOROGORO
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ELIDA LUHANGANO NDONDOLE
TANGAZO
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 Mwezi 7 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 4 mwezi 7 mwaka 2024

HAKIMU

---

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**FARAJI AJALI NENDAKUTOHA** anatangaza kupotelewa kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE417290** iliyotolewa uhamiaji makao makuu .kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/UBU/134554/2024**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**ISMAIL JUMA ZUBER MATAR** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1936-8861 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya HANANASIF mwaka 2019,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa PHQ/DAR/KIN/70523/2024**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACQUELINE MWELINDE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0232/0067/2011 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia HEKIMA GIRL'S SECONDARY SCHOOL mwaka 2011. kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: MWA/IGO/RB/299843/2022**

---

THE REGISTRATION OF DOCUMEMTS ACT (CAP 11 R . E. 2019)
DEED POLL ON CHANGE OF NAME

BY THIS DEED, I the undersigned JONATHAN DIGULA AMOS of Arusha -Tanzania , do hereby wholly, absolutely and utterly renounce , relinguish and abandon the use of my former names of JONATHANI AMOS DIGULA, as appearing in my Nationaly Identity Card,and adopt as from the date of this Poll and in substituation of my name, the names of JONATHAN DIGULA AMOS as appearing in my Academics certificates and Birth Certificate.

FOR THE PURPOSES OF evidence of such determination , I HEREBY DECLARE , that I shall at all times in future, in all records , deeds and instruments in writing and in all actions,proceedings dealings and transactions upon all occasions whatsoever use and sign the assumed name of JONATHAN DIGULA AMOS,instead of the name renounced .

The reason for the change is that, I want to be identified by similar name in all records and documents .AND I HEREBY AUTHORISE and request all persons to address me by such assumed name instead of the names renounced .

**DECLARED and SIGNED at ARUSHA by**
**The said JONATHAN DIGULA AMOS**
**Who is known to me personally }..** ..........................
**DEPONENT**
**This 27th day of JUNE 2024**
**BEFORE ME:**
**NAME JACKLINE OCTAVIUS LEOLE**
**SIGNATURE ..........................**
**ADDRESS P.O.BOX 470 ARUSHA**
**QUALIFICTION: COMMISSIONER FOR OATHS**



---

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**JUMAA SALIMU JUGWE**

anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki zenye usajili MC813 DRY,MC464 DNC,MC943 DLR,MC939 DFS,MC821 DDS,MC600 DCP, MC905 CYM. Kwa yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote Cha polisi kilichopo karibu nae.

TAARIFA YA POLISI:

**PHQ/TAN/MKI/6756/2024**

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 13586 OF 2024
In the matter of the Estate of the late JUMA GERSON MUTAFUTA of Mnadani ward
Within Dodoma City.
AND
In the matter of an application for Letters of administration by MARY HATSON KOTA.
GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)

**ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioners.**

**Objections to the grant should be filed on or before the 24 Day of 7 ...................... 2024**

**Dated at Dodoma this 06 Day of 06................2024**

**..........................................................................**
**PETITIONER**

**Presented for filing this 4......day of 7..........................2024**

**..........................................................................**
**RESIDENT MAGISTTRATE**

---

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO. 15034 OF 2024

In the Matter of the Estate of the Late:
MATHIAS JOHN MWIMBILIZYE

**By 1: MICHAEL MATHIAS MWIMBILIZYE**
**2: _______________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 18TH day of JULY.2024

Dated at MOROGORO this 27TH day of JUNE.2024

RESIDENT MAGISTRATE

---

IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
(DODOMA SUB REGISTRY)
PROBATE & ADMINISTRATION CAUSE NO. 6513 OF 2024
In the matter of the estate of the late LALJI THAWER of Dodoma City
And
In the matter of Application of Letter of Administration by PARVIZ MOHAMEDALI LALJI THAWER
GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 23rd day of July...................... 2024.

Dated at Dodoma this 23rd day of May................2024

... DEPUTY REGISTRAR ...

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**PIENSIA FOCUS NGURUWE**

anatangaza kupotea pikipiki aina ya BOXER zenye namba za usajili MC 800 DMR na MC 375 DQB. Kwa yeyote atakaeziona atoe tarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KIG/133631/2024**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RONALD MACHANGE WILLY**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI T103 BZW CHASISI NAMBA ET1965059768, RANGI NYEUPE AINA YA TOYOTA CALDINA,KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/9478/2024.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHABANI HALIBU RAJABU** Anatangaza kupotelewa na cheti cha Kidato cha nne chenye index namba S.000282188 kilichotolewa na Baraza la mitihani kupitia shule ya Sekondari ya Himo Secondary School Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa polisi: PHQ/ KIL/MOS/RB/14991/2024**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TUZIE KILALO MPOKERA**

anatangaza kupotea kw akdi ya gari yenye usajili namba T 664 DZE . kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chocote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KIN/114439/2024**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**YASIR OMARY ALLY** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA YENYE NAMBA TAE535459 ILIYOTOLEWA NA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA ,HIVYO KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA HATI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA PHQ/DAR/ILA/36053/2024.

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA/KIMATAIFA

# CCM yapongeza Aweso kusimamisha vigogo DAWASA

**Na Romana Mallya**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimebariki hatua iliyochukuliwa na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso ya kusimamisha kazi vigogo wawili wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kikisema, kuna watu wanataka kukichonganisha chama hicho kwa wananchi kwa makusudi.

Juni 30, mwaka huu, Waziri Aweso aliagiza Bodi ya Mamlaka DAWASA kuwasimamisha kazi Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu, Kiula Kingu na Mkurugenzi wa Uzalishaji na Usambazaji Maji wa mamlaka hiyo, Shaban Mkwanywe, kupisha uchunguzi.

Katibu wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM Taifa, Amos Makalla, aliyasema hayo jana katika ziara ya siku saba kwa kutembelea mradi mkubwa wa maji eneo la Bangulo, Jimbo la Ukonga, Halmashauri ya Manispaa ya Wilaya ya Ilala.

Mradi huo wa lita milioni tisa unagharimu Sh. bilioni 36, utakapokamilika mwezi Desemba mwaka huu, unatarajia kuhudumia wananchi zaidi ya 400,000.

"Ninampongeza Waziri Jumaa Aweso kwa ufuatiliaji wake na hata tumbuatumbua aliyofanya ni yale wale wanaotaka kutuchonganisha na wananchi, hivyo amefanya vizuri kwani kuna watu wanatuchonganisha na wananchi kwa makusudi," alisema.

Makalla alisema tangi hilo ambalo linachukua maji kutoka Ruvu Juu, litatatua kero katika maeneo yote korofi ambayo yamekuwa hayana huduma hiyo.

"Mambo ya maji ni ya wananchi yanalenga kumtua ndoo mama kichwani. Mradi huu ukamilike kweli mwezi Desemba kwakuwa mwakani tuna jambo letu tuwaambie hiki ndio chama kinachopanga na kinatekeleza, hata tunapokwenda kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa tunatakiwa kuwaaminisha kwamba, sisi mlitupa dhamana tumeahidi tunatekeleza," alisema.

Aliitaka DAWASA kufanya kazi ili jambo hilo likamilike kwa muda uliopangwa.

"Maana Waziri wa Maji (Aweso) aliuliza jambo la msingi siku ile, maji Ruvu Juu yapo, (akajibiwa) yapo. Lita ngapi yanaingiza, zikaelezwa. Kwa hiyo yapo ya uhakika (akajibiwa) ndio.

"Twende kwenye tangi la Chuo Kikuu, (akauliza) maji hapa yanaingia (akajibiwa) hayaingii, (akauliza) kwa nini wakati kule uliniambia maji yapo," alisema.

Makalla alisema kwa kauli hizo hata mtu anapowajibishwa hakuna huruma kwa kuwa inaonekana ni uzembe wa kiufundi na wa kutimiza majukumu.

"Ninaomba sana sisi tuna dhamana na wananchi jana (juzi) nilisema hakuna namna CCM isihusishwe na matatizo ya wananchi kwa kuwa ndio tulinadi Ilani tukapewa dhamana. Mambo yatakayofanywa yawe mazuri ni sifa kwa CCM, yakifanywa vibaya ni maneno kwa CCM," alisema.

Makalla alisema ni sahihi kabisa alichokifanya waziri kwa kuwa ameuliza maswali magumu akajibiwa majibu rahisi.

"Kwa hiyo msituchonganishe na wananchi wametuamini tunataka waendelee kutuamini, fanyeni kazi kwa bidii timizeni majukumu yenu. Hii tumbuatumbua aliyofanya hapa ametusaidia, mwananchi anakwambia umekuja maji yapo, lakini tulikuwa tunakunywa maji ya chumvi, je, watu wanafanya kusudi. Hongera sana Jumaa Aweso," alisema Makalla.

Waziri huyo aliwasimamisha kazi viongozi hao baada ya kufanya ziara katika maeneo la Chuo Kikuu cha Ardhi, Mbezi, Mshikamano na Tegeta A ambako kuna matangi ya maji.

Katika ziara yake jana, Makalla alitembelea pia, mradi wa mapitio ya stendi yaliyoko Chanika ambayo ujenzi wake unaendelea na baadae kufanya mkutano wa hadhara.

## Shambulizi laua 16 Gaza

**GAZA,** Palestina

SHAMBULIZI la kutisha la anga lililofanywa na jeshi la Israel, katika majengo ya shule moja jana limeua watu 16 na idadi kubwa wamejeruhiwa.

Shambulizi hilo lililenga shule iliyoko katika kambi ya wakimbizi katika ukanda wa Gaza.

Maofisa wa Palestina walisema jengo hilo lilikuwa likihifadhi maelfu ya watu waliokimbia makazi yao katika kambi ya wakimbizi ya Nuseirat katikati mwa Gaza.

Jeshi la Israel (IDF) lilisema liliwashambulia magaidi kadhaa waliokuwa wakiendesha shughuli zao katika majengo yaliyo katika eneo la Shule ya Al-Jaouni.

Wakati huo huo, kumekuwa na ripoti kwamba watu 10 waliuawa katika shambulio tofauti la anga kwenye nyumba moja katika kambi hiyo.

Video kutoka eneo la tukio iliwaonyesha watu wazima na watoto wakipiga kelele huku wakikimbia katika barabara iliyojaa moshi na vumbi la vifusi na wengine wakikimbia kusaidia majeruhi.

Watu walioshuhudia tukio hilo waliambia BBC kwamba shambulio hilo lililenga ghorofa za juu za shule hiyo, ambayo iko karibu na soko lenye shughuli nyingi.

Shirika la habari la Uingereza BBC lilisema kuwa watu 7,000 walikuwa wakitumia jengo hilo kama makazi.

Mwanamke mmoja aliambia shirika la habari la AFP jinsi baadhi ya watoto walivyouawa wakati walipokuwa darasani wakisoma Quran, pale jengo hilo liliposhambuliwa.

"Hii ni mara ya nne wanalenga shule bila kutoa onyo," alisema.

Chanzo cha ndani kilisema lengo lilikuwa chumba kinachodaiwa kutumiwa na polisi wa Hamas. Hata hivyo, hakuna uthibitisho wa dai hilo.

Kundi la Hamas lilisema kuwa waandishi wa habari watano wa ndani ni miongoni mwa waliouawa katika mashambulizi ya Israel yaliyofanyika Jumamosi. **IDF**




Viongozi wa nchi za AES wakiwa katika mkutano wa kwanza uliofanyika nchini Niger jana. **PICHA: RFI**

# Washikiliwa tuhuma kuiba nyaya njia SGR

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kuiba nyaya za shaba za njia ya Reli ya Mwendokasi (SGR) kipande cha Morogoro - Kilosa kuelekea Dodoma kinachoendelea kutengenezwa.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukagua kipande cha Morogoro hadi Kilosa akiwa ameambatana na wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya mkoa, alisema inashangaza kuona serikali inawekeza kwa ajili ya kuwasaidia wananchi, lakini wapo ambao hawafurahii mafanikio ya uwekezaji huo.

"Kuna watu wanapitapita kwenye njia ya reli ya SGR wamekamatwa watu watatu wakijihusisha na wizi wa nyanya nyeti za shaba, hii ni tabia chafu na mbaya sana," alisema Malima.

Bila kutaja majina ya watuhumiwa hao, Malima alisema SGR yenye maslahi ya Watanzania wote haibagui mtu, kabila, itikadi, dini na wote wananufaika na jambo hilo hivyo ni lazima wananchi waitunze kwa gharama yoyote.

"Hao wanaopanga kwenda kuhujumu miundombinu ya reli hii na kukata nyaya ili kupata shaba ninawapa salamu kuwa serikali haitokubali jambo hilo na watakaokamatwa hatua dhidi yao zitachukuliwa na kuwa mfano kwa wengine," alisema Malima.

Alisema, treni ya mwendokasi inawanufaisha Watanzania zaidi ya milioni 65, lakini kuna watu wachache wasioitakia mema nchi wanataka kurudisha nyuma maendeleo yaliyofikiwa kwa uwekezaji uliofanywa.

Aliutaka mkoa huo watu wasifanye masihara ya kuhujumu miundombinu ya reli hiyo katika maeneo ya Ngerengere hadi Kidete wilaya ya Kilosa.

"Tutawatafuta popote pale walipo wale wote watakaobainika kujihusisha na wizi wa miundombinu ya SGR na kuwakamata ili wafikishwe mahakamani na itakuwa ni fundisho kwa wengine wenye lengo la kuendelea kufanya hujuma hizi," alisema Malima.

Aidha, alisema hivi sasa vyombo vya ulinzi na usalama vya mkoa huo vipo macho kuhakikisha vitendo vya aina hiyo vinakomeshwa.

Katika hatua nyingine, aliwaomba wananchi wanaotumia usafiri wa SGR kuzingatia usafi wa mazingira kwenye eneo la vituo vya abiria na ndani ya treni hiyo.

Mkuu wa mkoa alisema hayo katika kituo cha SGR Kihonda, Manispaa ya Morogoro baada ya kuwasili na usafiri huo kutoka Dar es Salaam akiwa na Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa.

"Niwaombe watumiaji wa treni yetu ya SGR kuzingatia suala la usafi, watu wanakunywa maji na kutupa chupa nje, kutupa vifungashio hili si jambo zuri, watambue unapokuwa na kitu kikubwa kama hiki cha kimataifa lazima tubadilike na hatuwezi kufanya mambo ya ajabu ajabu," alisema Malima.

Mmoja wa abiria kutoka Dar es Salaam, Yusuf Mohamed, mkazi wa Morogoro alipongeza uwekezaji wa serikali kwa treni hiyo kuwa inasaidia kuwahi kwenye shughuli zao za kila siku.

Mmoja wa abiria, Tumaini Masige alisema alipangiwa kuonana na daktari saa nane mchana Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kutokana na huduma hiyo ilimsaidia kufika kwa wakati na kumaliza shida yake na kurudi Morogoro.

Alisema kuwa usafiri wa treni hiyo ni mkombozi kwa Watanzania na kwake umemsaidia kupunguza gharama ya kulala Dar es Salaam iwapo angetumia usafiri wa basi.

# TANGAZO

## KUPOTEA KWA CHETI



**FRANK GAITAN NGASSAPA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne cha K.S.C K.II. kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **REF/RMB/BI/38/VOL/192/06**

**IN THE DISTRICT OF KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.15447 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE NEGRO JACOB SANGA**

**AND**

**In the matter of Application for letters of Administration by:-**
**JEMA ELISHA KYANDO.........................PETITIONER**

**GENERAL CITATION (Rule 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 15 day of Jul, 2024

Dated at Kyela, this 1st day of July, 2024.

DISTRICT COURT KYELA TANZANIA

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE I/C
KYELA.

## KUPOTEA KWA CHETI



**SALUMU RAJABU MBONDE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4768/0058** kilichotolewa na baraza la taifa kupitia **KISIJU PWANI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **991083906575**

## KUPOTEA KWA VYETI



**YUSUPH NASSORO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P.1094.0078.2014** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ALDERSGATE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0496/0967/2017** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupititia JITEGEMEE SECONDARY SCHOOL **mwaka 2017 na** cheti cha chuo/bachelor chenye majina YUSUPH NASSORO ZAHORO chenye usajili namba **IMC/BIR/17/94234** kilichotolewa na **INSTITUTE OF FINANCE MANAGEMENT** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaevioana atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIG/49182/2023**

## CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI ZA MITAA TANZANIA (TALGWU)

# TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU) anawatangazia nafasi za ajira katika kada mbalimbali kama ifuatavyo:-

**1.0 AFISA MANUNUZI MWANDAMIZI TLGS F (Nafasi 1)**

**1.1 Sifa na uzoefu**

i. Awe na shahada ya kwanza katika fani ya Manunuzi au Ugavi kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
ii. Awe na cheti kutoka katika Bodi ya Manunuzi au ugavi
iii. Awe na uzoefu wa kufanya kazi za manunuzi au ugavi kwa kipindi kisichopungua miaka sita (6)
iv. Awe na ufahamu wa matumizi ya kompyuta
v. Mwanachama wa TALGWU atapewa kipau mbele
vi. Awe na umri usiozidi miaka 45

**1.2 Kazi za kufanya.**

i. Kukusanya takwimu za kusaidia kutayarisha makisio ya vifaa vinavyohitajika na Mpango wa Ununuzi (Procurement plan)
ii. Kuratibu na kusimamia masuala yote yanayohusu zabuni katika Chama.
iii. Kukusanya na kutunza takwimu za Wazabuni mbalimbali katika Chama
iv. Kukusanya na kutunza takwimu za upokeaji, utunzaji na usambazaji vifaa
v. Kubuni mfumo mzuri wa uwekaji na utunzaji wa vifaa vya Chama
vi. Kusimamia ukaguzi wa kihesabu wa vifaa vya Chama mara kwa mara
vii. Kutayarisha taarifa za kazi katika mwezi, robo mwaka na kila mwaka
viii. Kuwa Katibu wa vikao vya kamati ya zabuni katika Chama
ix. Kufanya kazi nyinginezo atakazopangiwa na Mwajiri wake

**2.0 AFISA MILIKI DARAJA LA II TLGS D (Nafasi 1)**

**2.1 Sifa na uzoefu**

i. Awe na shahada ya kwanza ya usimamizi wa ardhi, uhandisi wa majengo, ukadiriaji majengo au mchumi wa majengo kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali.
ii. Awe na uzoefu wa kufanya kazi za Afisa Miliki kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu (3)
iii. Ni lazima awe amesajiliwa na bodi ya kitaaluma
iv. Mwanachama wa TALGWU atapewa kipaumbele
v. Awe na ufahamu wa matumizi ya kompyuta
vi. Awe na umri usiozidi miaka arobaini na tano (45)

**2.2 Kazi za Kufanya**

i. Kuhakikisha viwanja na nyumba zote pamoja na majengo ya Chama yanatunzwa na kuwa kwenye hali nzuri
ii. Kupanga na kutoa ushauri wa namna nzuri ya kufanyia maboresho ya nyumba, Ofisi na majengo ya vitega uchumi.
iii. Kufuatilia ukarabati wa miundo mbinu yote ya majengo ya Chama
iv. Kuhakikisha usalama wa viwanja na majengo ya Chama baada ya kufanya matengenezo makubwa au kazi za ukarabati.
v. Kuhakikisha kazi za ukarabati na ujenzi zinafanyika kwa ufanisi, gharama nafuu na kukamilika kwa wakati.
vi. Kuandaa mpango wa uendelezaji wa rasilimali ardhi katika Chama
vii. Kumshauri mkuu wake katika mambo yote yanayohusu mali za Chama.
viii. Kusaidia katika shughuli za usimamizi wa miradi ya Chama
ix. Kufanya kazi zingine zote atakazopangiwa na mkuu wake.

**3.0 MRATIBU WA WILAYA DARAJA LA II TLGS B (Nafasi 4)**

**3.1 Sifa na uzoefu**

i. Awe na elimu angalau ngazi ya stashahada katika fani yoyote ile kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali.
ii. Awe na weledi mkubwa kuhusu vyama vya wafanyakazi na majukumu yake
iii. Awe na uelewa mpana kuhusu sheria na kanuni mbalimbali zinazotawala utumishi wa umma nchini.
iv. Awe na ufahamu wa matumizi ya kompyuta
v. Mwanachama wa TALGWU atapewa kipaumbele
vi. Awe na umri usiozidi miaka 45

**3.2 Kazi za kufanya**

i. Atakuwa ndiye mratibu wa shughuli zote za Chama Wilaya na atafanya kazi chini ya uongozi wa kamati ya uratibu ya Halmashauri.
ii. Atafuatilia kwa karibu utendaji kazi wa matawi yote yaliyomo wilayani na kuishauri kamati ya uratibu na Mkoa juu ya hatua kuchukua.
iii. Atakuwa ndiye mratibu wa vikao vyote vya Chama katika Wilaya.
iv. Kwa kushauriana na uongozi wa kamati ya uratibu ataitisha vikao vyote vya kamati kwa mujibu wa katiba ya Chama.
v. Atakuwa ndiye mratibu wa masuala yote yanayohusu mipango na bajeti katika Wilaya.
vi. Atakuwa mmoja ya watia saini katika nyaraka za kutolea fedha benki na kwa kushirikiana na Katibu wa Kamati ya uratibu.
vii. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha kwenye ngazi husika.
viii. Atawasilisha kwa Katibu wa Mkoa taarifa za kazi za Chama zilizopitishwa na vikao ngazi ya Wilaya
ix. Kuwa kiungo kati ya ngazi ya Wilaya na Mkoa
x. Kuratibu uanzishwaji wa matawi mapya sehemu za kazi katika Wilaya husika.

**4.0 NAMNA YA KUTUMA MAOMBI**

Waombaji wenye sifa zilizotajwa watume maombi yao kwa:

**Katibu Mkuu**
**Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU)**
**S.L.P 16097**
**DAR ES SALAAM**

NB: Barua zote za maombi ni lazima ziambatanishwe na wasifu (CV) wa muombaji, picha moja "passport size" ya hivi karibuni. Na nakala zilizothibitishwa za viwango vya ufaulu na vyeti vya taaluma. Majina matatu ya wadhamini yaonyeshe anuani na namba zao za simu. Maombi yatumwe kwa njia ya posta.

Pia tangazo hili linapatikana kwenye Tovuti ya TALGWU **www.talgwu.or.tz**

Mwisho wa kutuma maombi ni siku kumi na nne (14) tangu tarehe ya tangazo hili.

.........................
**Rashid M. Mtima**
**KATIBU MKUU – TALGWU TAIFA**

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ZIRKZEE FRESH MAN UNITED

KLABU ya Manchester United imekubaliana maslahi binafsi na mshambuliaji wa Uholanzi, Joshua Zirkzee, na wako kwenye mazungumzo na Bologna kuhusu jinsi klabu hiyo ya Italia inataka kiasi cha kuruhusiwa kuondoka kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(CaughtOffside)***

### LUKAKU KUTOLEWA

CHELSEA iko tayari kuwatoa mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 31, na kiungo wa kati wa Italia, Cesare Casadei mwenye umri wa miaka 21, kwa Napoli ili kusaidia kupunguza bei ya mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25. (***Teamtalk***)

### ARSENAL, CALAFIORI BADO

ARSENAL bado haijafikia bei ya Bologna ya pauni milioni 42.3 kwa ajili ya kumnunua mlinzi wa Italia, Riccardo Calafiori mwenye umri wa miaka 22, na mazungumzo kati ya klabu hizo mbili yanaendelea. ***(Football Italia)***

### ROYAL ATAKIWA MILAN

AC Milan imetoa ofa ya awali kwa beki wa kulia wa Tottenham Hotspur na Brazil, Emerson Royal lakini kuna pengo kati ya tathmini ya klabu kuhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Sky Sports Italia)***

### GROSS HUYOOO DORTMUND

KIUNGO wa kati wa Ujerumani, Pascal Gross, amekubali maslahi binafsi na Borussia Dortmund, ambao wako kwenye mazungumzo ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, kutoka Brighton kwa kati ya pauni milioni sita. ***(Sky Sports Germany)***

### GALLAGHER ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imehusishwa na kiungo wa kati wa Chelsea, Conor Gallagher mwenye umri wa mkaka 24, lakini mchezaji huyo wa Kimataifa wa England hana uwezekano wa kuhamia Spurs msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### ALMIRON KUPIGWA BEI

WINGA wa Newcastle United, Miguel Almiron yuko kwenye mazungumzo na mwakilishi wake kuhusu mustakabali wake huku mchezaji huyo wa Kimataifa wa Paraguay mwenye umri wa miaka 30, akihusishwa na kuhamia Saudi Arabia na 'Magpies' wanaaminika kuwa tayari kumuuza. ***(Chronicle)***


### MORATA KUBAKI ATLETICO

MSHAMBULIAJI wa Hispania, Alvaro Morata, anatafakari iwapo ataondoka Atletico Madrid na kujiunga na AC Milan, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, akisema atasalia katika klabu hiyo ya Hipania hadi ashinde nao kitu. ***(Corriere dello Sport)***

### WIRTZ SASA AGOMBEWA

REAL Madrid ina imani kuwa inaweza kuwashinda wapinzani wao, Barcelona katika kumsajili kiungo wa kati wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Florian Wirtz, 21. ***(Sport)***

## DOND ZA SOKA MAG ULAYA



# SAKA: NAJIVUNIA ENGLAND KUTINGA NUSU FAINALI EURO

**BERLIN,** Ujerumani

BUKAYO Saka, ambaye alikosa penalti katika mechi ya fainali ya Euro 2020 dhidi ya Italia na baadaye akawa mwathiriwa wa ubaguzi wa rangi, alikuwa shujaa wa England kwa bao kipekee na mkwaju wa penalti dhidi ya Uswisi katika robo fainali ya Euro 2024 Jumamosi.

**Saka ambaye aliifungia England bao lao muhimu la kusawazisha, alisema anajivunia jinsi alivyoshinda wakati huo.**

"Kurejea kutoka kwa kitu kama hicho ilikuwa ngumu sana. Niliitumia kunifanya kuwa na nguvu zaidi. Leo (juzi) nilichukua nafasi hiyo na nina furaha," alisema winga huyo wa Arsenal.

> ●●● Ilikuwa maalum, mara ya mwisho Euro tulipiga penalti mnajua kilichotokea...

"Ilikuwa maalum, maalum, jinsi tulivyopambana ... mara ya mwisho tulipiga penalti kwenye Euro, wote mnajua kilichotokea. Ninajivunia kila mtu jinsi tulivyovuka mstari.

"Niliamini. Nilihisi kwamba tulitawala mchezo mzima, kwamba nafasi ya bao itakuja. Na ilikuja na mimi ndiye niliyeichukua, kwa hivyo ninajivunia kwa hilo."

Sasa Saka ni mtu maarufu na, akiwa na umri wa miaka 22, ameichezea timu ya taifa mechi 38 na kifunga mabao 12.

Mechi ya Jumamosi inaweza kuwa ya kipekee kuliko zote.

Saka alifunga bao la kusawazisha wakati England ilipokuwa nyuma kwa 1-0 katika robo fainali dhidi ya Uswisi. Kisha, mchezo ulipomalizika kwa 1-1 baada ya muda wa ziada, alikuwa mmoja wa wafungaji watano wa penalti wa England katika ushindi wa 5-3.

"Saka ni jasiri sana," alisema Southgate baada ya England kushinda na kukata tiketi ya nusu fainali, ambapo watamenyana na Uholanzi Jumatano.



# KROOS AMUOMBA RADHI RAFU

**BERLIN,** Ujerumani

TONI Kroos ameomba msamaha kwa Pedri kwa changamoto iliyohitimisha kampeni ya kiungo huyo wa Hispania kwenye Euro 2024.

Katika kile kilichoishia kuwa mechi ya mwisho ya maisha ya Kroos, alimfanyia madhambi Pedri katika dakika za mwanzo za mchezo.

Licha ya juhudi zake za kuendelea, kinda huyo wa Barcelona hatimaye alilazimika kuondoka uwanjani baada ya dakika nane pekee. Kocha wa Hispania, Luis de la Fuente, amedai Kroos alipaswa kupewa kadi nyekundu kwa changamoto hiyo, na kiungo huyo wa zamani wa Real Madrid sasa ameomba radhi kwa tukio hilo.

Katika kuaga kwake akiwa anastaafu soka, Kroos aliandika: "Hili ni muhimu kwangu. Ninaomba msamaha kwa Pedri! Ni wazi, sikukusudia kukuumiza. Upone haraka na kila la heri. Wewe ni mchezaji mkubwa."

Pedri alipelekwa haraka kuchunguzwa jeraha hilo, jambo ambalo Barcelona walihofia huenda hayuko tayari kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya. Kwa mujibu wa gazeti la Mundo Deportivo, Pedri amegundulika kuwa na mpasuko katika goti lake la kushoto jambo ambalo litamfanya kuwa nje kwa kati ya wiki nne hadi sita.

Ina maana Pedri atakosa kampeni ya kwanza ya Barcelona ya kujiandaa na msimu mpya chini ya kocha mpya, Hansi Flick. Ziara ya Marekani italeta mechi dhidi ya Manchester City, Real Madrid na AC Milan kabla ya Agosti 6, lakini Pedri atalazimika kutazama akiwa jukwaani.

Wakati huo huo, Pedri anatarajiwa kusalia na kambi ya Hispania kwa mapumziko ya safari yao ya Euro 2024, ambayo inaendelea na mchuano wa nusu fainali dhidi ya Ufaransa Jumanne.

# Nyota wa Misri afariki dunia

**CAIRO,** Misri

MCHEZAJI wa Kimataifa wa Misri, Ahmed Refaat, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 31, klabu yake ya Modern Sport Jumamosi ilisema ni baada ya mshtuko wa moyo alioupa Machi wakati wa Ligi Kuu Misri.

Refaat aliwekwa katika chumba cha wagonjwa mahututi mnamo Machi 11, mwaka huu baada ya kuzimia katika dakika ya 88 ya mechi ya Ligi ya Modern Future dhidi ya Al-Ittihad Alexandria.


Mshambuliaji huyo ambaye alikuwa amewekewa kifaa cha kusaidia mapigo ya moyo, aliruhusiwa mwezi mmoja baadaye na kuendelea kupata matibabu.

"Modern Future FC inatangaza kifo cha Ahmed Refaat, mchezaji wa kikosi cha kwanza na Timu ya Taifa ya Misri, kutokana na kuzorota kwa afya yake," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

"Alihamishiwa hospitalini baada ya safari ya kupambania afya yake kutokana na mzoroto wa kiafya uliotokea Machi 11 2024."

Nahodha wa Misri na mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, alitoa salamu za rambirambi kwa mchezaji mwenzake huyo Refaat, ambaye aliichezea timu ya taifa mara saba na kufunga mabao mawili.

"Mungu aendelee kubariki familia yake na wapendwa wake wote," aliandika Salah kwenye X.





# *Dorival abeba lawama kutolewa Copa America*

**LAS VEGAS,** Marekani

KOCHA wa Brazil, Dorival Junior, amesema anachukua "jukumu kamili" kwa timu yake kutolewa kwenye robo fainali ya Copa America dhidi ya Uruguay iliyokuwa na wachezaji 10 kwa penalti 4-2 Jumamosi.

"Kazi ya aina hii inahitaji uvumilivu mkubwa," alisema Dorival, ambaye alichukua jukumu la kuinoa timu hiyo Januari baada ya kushindwa kwenye Uwanja wa Allegiant.

"Lazima nikubali kwamba haya hayakuwa matokeo yaliyotarajiwa, na ninachukua jukumu kamili kwa ajili yao, lakini nadhani vile vile kuwa timu hii ina nafasi nzuri ya kukua na kubadilika na kuboreshwa."

Licha ya kuwa na faida ya mchezaji mmoja baada ya kadi nyekundu aliyopewa Nahitan Nandez wa Uruguay dakika ya 74, Brazil ilishindwa kufurukuta baada ya mechi kali iliyohusisha faulo 41 kumalizika kwa suluhu baada ya dakika 90 na kwenda mikwaju ya penalti.

Katika mikwaju ya penalti, Eder Militao na Douglas Luiz walishindwa kuzifumania nyavu za Brazil, huku Alisson Becker akimnyima kufunga beki wa Uruguay, Jose Maria Gimenez.

Hata hivyo, Manuel Ugarte alifunga mkwaju wa penalti wa ushindi na kupeleka Uruguay katika hatua ya nne bora na Brazil kuondolewa.

Brazil wanarejea nyumbani baada ya kupata ushindi mmoja pekee katika hatua ya makundi kabla ya kushindwa na Uruguay katika raundi ya kwanza ya mtoano.

Matokeo pia yanawakilisha zamu ya chini kwa Wabrazil, ambao walikuwa washindi (2021) na mabingwa (2019) katika matoleo mawili ya awali ya Copa Amerika.

"Huu ni mchakato; kwa ujumla, unakutana na matatizo unapounda timu," alisema Dorival, ambaye timu yake haikuwa na Vinicius Junior aliyesimamishwa katika robo fainali.

"Haya yalikuwa mashindano yetu ya kwanza rasmi, na matokeo yalikuwa mbali na ilivyotarajiwa ... lengo letu kuu sasa ni kufuzu kwa Kombe la Dunia."

Dorival, ambaye ana mechi nane pekee, aliwatetea wachezaji wake.

"Wengi wao walijiunga nasi baada ya misimu mirefu," Dorival alisema.

"Kwa kuzingatia tulivyoona kwenye vikao vya mazoezi na kila siku, nadhani bado tunaweza kukua kama timu... watu wengi wanaweza wasielewe, mambo ni kama haya wakati unaunda timu kutoka mwanzo. Kuna kupanda na kushuka. katika soka."

HABARI MICHEZO

## Kazini kwa Tshabalala shughuli pevu

INATOKA UKURASA 24

ya nchi, Klabu ya Simba, pamoja na masuala ya fedha.

"Ilikuwa ni semina ya kuwandaa kisaikolojia, wachezaji wameambiwa historia ya Simba na nchi ya Tanzania, ukubwa wa klabu, vitu ambavyo imeshawahi kuvifanya huko nyuma na malengo yake ya baadaye," alisema Ahmed.



Wakati huo huo, Mwekezaji, Rais wa Heshima na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mohamed 'Mo' Dewji, alikuwa na kikao kizito na Bodi ya Wakurugenzi ya Klabu, pamoja na ya ile ya ushauri ambayo aliiteuwa mwenyewe Oktoba 23, mwaka jana.

Imeelezwa, pamoja na mambo mengine, ilikuwa ni kujadili mwenendo wa timu msimu uliopita, pamoja na kupanga mikakati ya kurudisha heshima ya klabu hiyo.

## Ligi Kuu Bara kuanza Agosti 17

INATOKA UKURASA 24

kufanya kazi, badala yake amewataka waamuzi kuwa makini zaidi katika kuchezesha vema, kwa uangalifu na kufuata sheria zote 17.

"Kingine ni kwamba pamoja na kuitumia, lakini bado haiwezi kumaliza tatizo, kwa sababu kwa mujibu wa FIFA yenyewe inasimamia mambo matatu, utata wa kadi nyekundu, kuotea na penalti, haihusiki na bao, mambo mengine wanawaachia waamuzi wenyewe, mfano mechi ya Yanga na Mamelodi Sundowns, watu wa VAR waliwaachia wenyewe kwa sababu siyo katika vitu ambavyo inapaswa kuviamua.

"Kwa maana hiyo pamoja na kuwepo kwa VAR, waamuzi bado wanatakiwa wawe makini na wachezeshe kwa uangalifu," alisema Kasongo.

# WASHINDI DODOMA MARATHON WATENGEWA SHILINGI MILIONI 82

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya washindi 60 wa mbio za Dodoma Marathon msimu huu wanatarajiwa kuondoka na zawadi zenye jumla ya thamani ya Sh. milioni 82 pamoja na medali, imefahamika.

**Mbio hizo zenye hadhi ya kimataifa zinatarajiwa kufanyika Julai 28, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma zikiwa na lengo la kukusanya fedha ili kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi na kutoa ufadhili wa elimu kwa wakunga ili kuboresha afya ya mama wa mtoto.**

Hafla ya utambulisho wa zawadi hizo ilifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki ikihusisha maofisa kutoka Benki ya NBC ambayo ndio inaratibu mbio hizo na wadau mbalimbali wa mchezo huo wakiwamo waandishi wa habari tukio lililoshuhudiwa na maelfu ya watazamaji kupitia vyombo mbalimbali vya habari vilivyokuwa vikionesha mubashara tukio hilo lenye mvuto wa aina yake.

Wakifafanua kuhusu zawadi hizo Meneja Mahusiano ya Umma na Mawasiliano wa NBC, Brendansia Kileo na Meneja wa Biashara ya Kadi wa benki hiyo, Esnat Holella, walisema viwango vya zawadi hizo vimeongezwa zaidi msimu wa mwaka huu ikiwa ni muendelezo wa jitihada za benki hiyo katika kuongeza hadhi ya mbio hizo kila mwaka.

Zaidi ongezeko hilo la viwango vya zawadi linatwaja kuwa linalenga kuchochea ushiriki zaidi wa wanariadha wengi wakiwamo wa kimataifa, hatua ambayo inalenga kuongeza ushindani zaidi kwa washiriki.

"Hivyo basi taarifa njema kwa washiriki wa Dodoma Marathon mwaka huu ni kwamba pamoja na medali kwa washiriki wote wa mbio hizi, washindi wa kwanza wa mbio za kilomita 42 kwa wanaume na wanawake watajinyakulia Sh. milioni 11.5 kila mmoja, Sh. milioni tano kwa washindi wa pili, Sh. milioni 2.5 kwa washindi wa tatu, Sh. milioni 1.5 kwa washindi wanne na Sh. milioni moja kwa washindi wa tano, huku washindi wa sita hadi kumi nao pia wakiibuka na zawadi na pesa taslimu," alisema Kileo

Kwa upande wa mbio za Kilomita 21, Kileo alisema pamoja na medali washindi wa kwanza kwa wanaume na wanawake watajinyakulia Sh. milioni 5.5 kila mmoja, Sh. Mil 2.5 kwa washindi wa pili, Sh. milioni 1.2 kwa washindi wa tatu, Sh. 750,000 kwa washindi wanne na Sh. 600,000 kwa washindi wa tano huku pia washindi wa sita hadi wa kumi wakiibuka na zawadi za pesa taslimu kila mmoja.

"Mbio za kilomita 10 washindi wa kwanza wanaume na wanawake watajinyakulia Sh. milioni 2.5 kila mmoja, Sh. milioni 1.5 kwa washindi wa pili, Sh. 750,000 kwa washindi wa tatu, Sh. 500,000 kwa washindi wanne na Sh. 400,000 kwa washindi wa tano, huku washindi wa sita hadi kumi nao pia wakiibuka na zawadi na pesa taslimu," aliongeza Kileo

Aidha, Kileo aliongeza kuwa vifaa maalumu vitakavyotumiwa na washiriki wa mbio hizo zikiwamo jezi vinatarajiwa kutolewa kwa washikiri katikati ya mwezi huu huku akiendelea kutoa wito kwa jamii kuendelea kujisajili na kuchangia kiasi cha Sh. 35,000 kwa usajili wa washiriki mmoja mmoja au 25,000 kwa usajili wa kikundi chenye idadi ya watu wanaozidi 25 ili kuunga mkono agenda kuu ya mbio hizo.

Kwa upande wa Holella, yeye aliwashukuru wadau mbalimbali wanaoendelea kujitokeza kushiriki maandalizi ya mbio hizo yakiwamo mashirika na kampuni mbalimbali wakiwamo Sanlam Insurance ambao ni wafadhili wakuu wa mbio hizo huku wadau wengine wakiwa ni Jubilee Allianz General Insurance, Garda World, Metropolitan, SGA,SBC, Benki za CRDB na NMB, Computech Solutions na Hans-Paul.




Maofisa waandaji wa Dodoma Marathon, Brendansia Kileo (wa pili kulia) na Esnat Holella (wa pili kushoto) pamoja na wadau wa habari akiwamo Eddo Kumwembe (katikati), Oscar Oscar (Kulia) na Adela Tillya (kushoto) wakionesha viwango vya zawadi fedha taslimu zitazotolewa kwa washindi mbalimbali wa msimu wa tano wa mbio hizo zinazotarajiwa kufanyika Julai 28, mwaka huu, Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma. **MPIGAPICHA WETU**

# *Dube sasa rasmi kuanza kuitumikia Yanga*

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE baada ya tetesi za muda mrefu, straika wa zamani wa Azam FC, Prince Dube, ametangazwa rasmi kuwa ni mchezaji wa Yanga.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imesema kuwa Dube kwa sasa ni mali ya Yanga na ataitumikia kuanzia msimu ujao wa mashindano.

"Juzi niliwaambia kuwa kila usajili wetu tutakaokuwa tukiutangaza utakuwa ni wa kutikisa nchi, tulianza wa Clatous Chama, ikawa balaa, sasa umekuja huu na Dube, nao umeanza kutikisa na kuwa gumzo, na bado tunaendelea kushusha vyuma, kuelekea msimu ujao tunataka kutengeneza timu ya kutisha, ya wachezaji ambao wanawaza kwenda kuchukua medali, lengo letu kuelekea msimu unaokuja ni kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, fainali, au kutwaa ubingwa kabisa," alisema," alisema Ofisa Habari ya Yanga, Ali Kamwe.

Kujiunga kwa straika huyo raia wa Zimbabwe kunamamilisha tetesi za muda mrefu kuwa alikuwa akitakiwa na klabu hiyo, baada ya kuwa na mgogoro wa kimkataba na klabu yake ya Azam.

Imeelezwa kuwa Dube amekuwa huru kujiunga na Yanga, baada ya kuilipa Azam kiasi cha Sh. milioni 500 alizokuwa akidaiwa.

Awali, Dube aliukana mkataba aliokuwa nao na Azam uliokuwa uishe 2026, na akasusa kiasi cha kutookena katika mechi nyingi za Ligi Kuu. Mchezaji huyo aliishtaki klabu yake na kesi ikasikilizwa, ambapo hukumu ilionyesha kuwa alikiuka makubalia yake kimkataba, hivyo kutakiwa kulipa fidia.

# Michezo

Jumatatu Julai 8, 2024

Nipashe




Klabu zinazohitaji saini ya Costa UKURASA 12

## LA KUCHOMOA!...



Mshambuliaji wa England, Bukayo Saka, akiifungia timu yake bao la kusawazisha wakati wakitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Uswisi kwenye mechi ya robo fainali ya michuano ya Euro 2024 iliyopigwa Ujerumani juzi na Waingereza kushinda kwa mikwaju ya penalti 5-3. **HABARI UK. 21. PICHA: MTANDAO**

# *Kazini kwa Tshabalala shughuli pevu Simba*

## ●●● Aletewa mashine ya kupanda na kushuka kama umeme, Mo aitisha kikao kizito, waenda Misri...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikitarajiwa kuondoka leo jioni kwenda Ismailia nchini Misri kwa ajili ya kambi ya wiki tatu kwa maandalizi ya msimu ujao mashindano, Klabu ya Simba imetangaza kumsajili beki wa kushoto raia wa Burkina Faso, akitokea FC Saint Eloi Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Valentin Nouma.

**Klabu hiyo ilimtangaza mchezaji huyo jana mchana katika mfululizo wa kutambulisha wachezaji wake wapya iliyowasajili kwa ajili ya kukitumikia kikosi hicho ambacho kinakabiliwa na michuano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.**

"Tumeendelea kushusha vyuma na bado tutaendelea, wanachama na mashabiki wa Simba waendelee kusubiri mambo mazuri, kusema kweli msimu ujao tutakuwa na kikosi bora sana," alisema Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally.

Kabla ya kujiunga na timu hiyo ya DR Congo, beki huyo alizichezea Klabu za Rahimo FC, AS Douanes zote za Burkina Faso.

Mchezaji huyo anatajwa kwenda kuwa mbadala wa beki wa sasa wa kikosi hicho, Mohamed Hussein 'Tshabalala' ambaye anadaiwa anacheza mechi nyingi bila kupumzika kutokana na kutokuwa na msaidizi wa kuaminika, hivyo sasa atakuwa na kazi ya kupigania namba na mchezaji huyo.

Mpaka sasa klabu hiyo imewatangaza wachezaji 10 wapya, sita wakiwa ni wageni na wanne wazawa, ambao ni Jushua Mutale kutoka Power Dynamos ya Zambia, Steven Mukwala akitokea Asante Kotoko ya Ghana, Jean Charles Ahoa kutoka, Stella Adjame ya Ivory Coast, Debora Fernandes Mavambo kutoka Mutondo Stars ya Zambia na Augustine Okajepha, kutoka Rivers United ya Nigeria.

Wachezaji wazawa waliotangazwa mpaka sasa ni Lameck Lawi kutoka Coastal Union, Abdulrazack Hamza wa Super Sports ya Afrika Kusini, Valentino Mashaka, akitokea Geita Gold na Omari Omari aliyekuwa akikipiga Mashujaa FC.

Wakati hayo yakiendelea, kikosi cha timu hiyo kinatarajiwa kuondoka leo jioni kuelekea Ismailia nchini Misri kwa ajili ya maadalizi ya msimu mpya.

Ahmed amesema kikosi hicho kitakuwa huko kwa muda wa wiki tatu kabla ya kurejea, tayari kwa mechi za tamasha la kila mwaka, Simba Day.

Kabla ya kuondoka nchini, wachezaji wote wa timu hiyo walipata semina ya mambo mbalimbali, ikiwamo masuala ya kisailolojia, kupewa historia

INAENDELEA UKURASA 23

# Ligi Kuu Bara kuanza Agosti 17

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/25, inatarajiwa kuanza rasmi Agosti 17, ikizishirikisha jumla ya timu 16 ambazo zitakuwa na kazi ya kusaka ubingwa na nafasi zingine tatu ambazo zitaziwezesha kucheza mechi za kimataifa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu, Almasi Kasongo, amesema Ligi Kuu itaanza katikati ya Agosti, wiki moja baada ya kumalizika kwa Ngao ya Jamii, Agosti 11.

Ingawa hakutaja tarehe rasmi, inaonyesha baada ya fainali ya Ngao ya Jamii kuchezwa siku hiyo ya Jumapili, wiki moja inayofuata ambayo itakuwa ni Jumamosi ya Agosti 17, mwaka huu.

"Tupo kwenye maandalizi ya ratiba, ligi yetu itaanza katikati ya mwezi wa nane, nadhani baada ya ile wiki ya mechi za Ngao ya Jamii, kuanzia tarehe hadi 11, basi wiki inayofuata inakwenda kuanza.

Ukiangalia ratiba, tarehe nane ni mechi ya kwanza, tisa ya pili, tarehe 10 mapumziko, 11 fainali, wiki moja tu baadaye ligi inaanza rasmi," alisema.

Alikumbusha kwa mara nyingine tena kuwa msimu ujao kwa mara ya kwanza Ligi Kuu itatumia teknolojia ya video ya kumsaidia mwamuzi (VAR), ingawa si kwa mechi zote.

"Msimu ujao tutakuwa na VAR, lakini niwaambie tu haitokuwa kwa michezo yote ya Ligi Kuu, ila itatumika kwenye michezo mingi tu ila haitokuwa asilimia 100," alisema.

Hata hivyo, Ofisa Mtendaji Mkuu huyo ameonya kuwa kuwapo kwa VAR hakutamaliza tatizo au changamoto zilizopo kwani ina maeneo yake tu ya

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >